MID WEEK JACKPOT!
TZS. 718,345,550
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

Jumatatu Septemba 25, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581444
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 7

**Waziri** Mkuu atoa siku tano kituo kipewe watumishi



UKURASA WA 8

**Jumuiya** Wazazi CCM yahadharisha tabia ya 'uchawa'



UKURASA WA 19

**Dhamira** ya Samia kuvutia uwekezaji yaundiwa mkakati



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu

RIPOTI MAALUM

# Hatari wanawake wanaotumia Fragyl kuzuia ujauzito

• **Udadisi** wa Nipashe wabaini wapo wanaomeza hadi vidonge 12 kwa siku, madaktari bingwa waonya... *Ukurasa 4*




## YALIYOMO

UKURASA WA 10

**JELA MIAKA MITANO KWA WIZI WA KINANDA CHA KANISA**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Sengerema imemuhukumu kwenda jela miaka mitano mkazi wa Mwabaruhi, Mussa Juma baada...

## Waziri ashtuka watoto kucheza sherehe za usiku, wadau wajipanga

UKURASA 3



## Wafugaji wacharuka operesheni ya kuwaondoa, DC atoa ufafanuzi

UKURASA 2

MICHEZO MWAMNYETO AAHIDI HISTORIA YANGA UK.24 KATUNI UK.6

# Biteko ataka uwajibikaji serikali za mitaa

**Na Jenifer Gilla**

NAIBU Waziri Mkuu, Dotto Biteko, amewataka watumishi wa halmashauri nchini kusimamia vyema fedha za miradi ya maendeleo ili ziwe na tija kwenye maisha ya wananchi wa ngazi zote.

Akiwa jimboni kwake Bukombe, mkoani Geita jana kwa ajili ya kuwashukuru wananchi tangu ateuliwa katika wadhifa mpya huo pamoja na kuwa Waziri wa Nishati, alisema fedha nyingi za serikali zinaelekezwa serikali za mitaa ambako kuna wananchi wengi.

Alisema ni muhimu fedha zikatumika kwa haki kwa ajili ya kuleta maendeleo ya wananchi na siyo kwa maslahi binafsi.

Alisema inasikitisha kuona fedha zilizotolewa kwa ajili ya maendeleo ya nchi zinaliwa na watu wachache au zinakaa kwenye akaunti bila kutumika kwenye miradi ya maendeleo ambayo inatatua changamoto mbalimbali za wananchi.

Alisema wakati anakwenda kumuaga Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuwa anakwenda kutembelea jimbo hilo alimwagiza awakumbushe watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe kusimamia fedha hizo ili zikatumike kuwakomboa wananchi kiuchumi.

Dk. Biteko alisema, Rais Samia anafanya kazi kubwa ya kuboresha maisha ya wananchi kwa kuidhinisha fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuwaagiza watumishi fedha hizo zitumike kihalali ili wasimwangushe.

"Mheshimiwa Rais amewafanya Watanzania wawe daraja la juu kwa fedha anazozimwaga kwa ajili ya maendeleo yao. Miradi inayozungumzwa sasa imekuwa jambo la kawaida kila anayesimama mahali popote anataja mabilioni ya fedha yanayopelekwa kwa wananchi," alisema Biteko.

Aliwasihi viongozi wa halmashauri hiyo kuanzia ngazi ya serikali ya mtaa hadi mawaziri wafanye kazi kwa bidii na ushirikiano kwa kuwa Watanzania wanaangalia na watawapima kulingana na utendaji kazi wao.

Aliwasihi wananchi wa halmashauri hiyo kupendana, kuthaminiana na kufanya kazi pamoja kuijenga halmashauri hiyo ili watoto wao waikute ikiwa bora na wasikubali itikadi za chama au dini kuwatenganisha.

Alimshukuru Rais Samia kwa kumpa heshima ya kuwa kuwa Naibu Waziri Mkuu, cheo kilichobeba majukumu na wajibu mkubwa wa kulitumikia taifa na kuahidi kufanya kazi kwa bidii kadiri Mungu atakavyombariki kuwaletea wananchi maendeleo.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alisema ataendeleza misingi mizuri iliyoachwa na waziri huyo wakati wa utendaji wake ili kuwaletea Watanzania maendeleo kupitia rasilimali madini.

Alisema moja ya mambo atakayofanya ni kutekeleza agizo alilotoa Rais Dk. Samia la kufanya utafiti kubaini maeneo yenye miamba ya madini ili wachimbaji wadogo wasifanye shughuli hiyo kwa kubahatisha.

Alisema pia kupitia Mfuko wa Dhamana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) watawapatia wachimbaji wadogo mitaji pamoja na kujadili na taasisi nyingine za fedha ili kuongeza nguvu ya kutoa mikopo kwa wafanyabiashara hao wapate mitaji na kuongeza kasi ya mitaji hiyo.

Mavunde alisema Biteko alifanya kazi kubwa ya kuinua sekta ya madini ikiwamo kupambana na utoroshaji wa madini na yeye ataendelezaalipoachia ili kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo.

"Baada ya hapo hatutokuwa na mswalie Mtume kwa mtu yeyote atakayefanya kazi ya utoroshaji wa madini na kulikosesha taifa letu la Tanzania mapato, hayo ndiyo yanayojenga hospitali na shule," alisema.



Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Muheza, Tanga, Leonard Bandora, akitoa elimu ya usalama barabarani juzi katika Kijiji cha Mpakani wilayani Muheza baada ya kupokea kero kwa wananchi wakiiomba serikali kuwajengea matuta eneo hilo na kuwekewa alama za barabarani Pundamilia na vibao vya spidi 50 baada ya watu 16 kupoteza maisha kwa kugongwa na magari. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wafugaji walaani operesheni inayoendelea, DC afafanua

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Wafugaji Tanzania (CCWT) kimelaani vitendo vya unyanyasaji na mauaji ya wafugaji vinavyodaiwa kufanyika hivi karibuni katika wilaya za Tunduru mkoani Ruvuma na Nachigwea mkoani Lindi.

Kutokana na hali hiyo, chama hicho kimemwangukia Rais Samia Suluhu Hassan kikimwomba kuingilia kati kwa kuunda tume itakayosaidia kukomesha hali hiyo kwa kuwa ni kero kwa wafugaji katika mikoa ya kusini.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Kusundwa Wamalwa, alibainisha hayo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu matukio ya mapigano kati ya wafugaji na wakulima katika wilaya hizo.

Alisema katika siku za karibuni kumekuwa na mapigano ya wakulima na wafugaji kwenye maeneo hayo na kusababisha baadhi ya wafugaji kupoteza maisha.

"Hivi karibuni kumekuwapo na mapigano ya kushtukiza katika maeneo haya ya wakulima na wafugaji ambayo yamepelekea baadhi ya wafugaji wetu kupoteza maisha tunaiomba serikali ichukue hatua kwa kuwa wafugaji wananyanyasika sana kana kwamba si Watanzania.

"Mnamo Agosti 4, 2023, kuna mfugaji aliyejulikana kwa jina la Weja Lukaresha, anadaiwa kufa katika Kijiji cha Chiwana, Tarafa ya Narasi wilayani Tunduru kwa kupigwa risasi akiwa ndani ya zizi la mifugo yake, lakini hakuna hatua ambazo zimechukuliwa hadi hivi sasa," alidai.

Kiongozi huyo alisema kuwa moja ya sababu zinachochea vitendo vya unyanyasaji wa wafugaji ni operesheni ya kukamata mifugo inayoendeshwa na mkuu wa wilaya ya Tunduru.

"Tumemwandikia barua Mkuu wa Wilaya ya Tunduru kusitisha operesheni hii na nakala kuipeleka katika wizara mtambuka ikiwamo Ofisi ya Rais - TAMISEMI, lakini hakuna hatua zilizochukuliwa," alisema.

Wamalwa alisema kuwa kutokana na operesheni hiyo kutumika vibaya na kamati za ulinzi na usalama imepelekea mifugo kumatwa na kushikiliwa na mkuu wa wilaya kwa muda mrefu.

"Wafugaji wananyanyaswa sana, wapo ambao wameombwa rushwa na wengine wamelipa faini, fedha nyingi ambazo malipo yanafanyika kinyume cha taratibu za serikali kwa kuwa hakuna namba ya malipo ya serikali wanayopatiwa kwa ajili ya malipo na walioshindwa mifugo yao imeshikiliwa hadi sasa," alisema.

Kiongozi huyo wa wafugaji alisema wanaishauri serikali kushirikiana na chama hicho ili kwenda katika maeneo hayo na kuzungumza na wafugaji kwa lengo la kupata suluhu ya kudumu ikiwamo utengaji maeneo ya nyanda za malisho.

"Hivi sasa wafugaji wanalazimishwa kwenda kwenye vitalu vilivyotengwa lakini maeneo hayo pamoja na wafugaji kulipa fedha hayana miundombinu. Mfugaji anatakiwa kuchimba kisima, gharama zake ni takribani milioni 20," alilalamika.

Kaimu Katibu Mkuu wa CCWT, Mathayo Daniel, aliomba mamlaka za nchi kuhakikisha yeyote aliyehusika na kifo cha mfugaji anachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

"Hatuelewi ni kwanini hadi sasa mamlaka zipo kimya na mhusika anafahamika. Tunaomba hatua zichukuliwe ili mfugaji yule aliyeuawa ndani ya zizi la mifugo yake kwa kupigwa risasi anapata haki yake," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, akifafanua kuhusu madai hayo wilayani mwake kwa waandishi wa habari, alithibitisha kuendelea kwa operesheni ya kuhamisha mifugo inayochungwa holela. Inapelekwa katika vitalu vilivyo tengwa.

"Tunatekeleza operesheni hii kwa mujibu wa sheria ili kuondoa ufugaji holela na kulinda maeneo yetu ikiwamo vyanzo vya maji, lakini wafugaji hawataki. Tumeshatenga vitalu 279 kwa ajili yao," alisema.

Kuhusu madai ya kufanyika mauaji wilayani mwake, Mtatiro alisema hakuna madhara yoyote yaliyosababishwa na operesheni hiyo.

"Chama cha wafugaji hawapendi operesheni yangu na mimi ni mdau wa mazingira. Siwezi kurudi nyuma kamwe, acha wanichukie ndiyo maana hata linapotokea tukio la mauaji wanasema ni kwangu, lakini hadi sasa kwangu ni shwari ila ninasikia katika wilaya nyingine ndiko yametokea mauaji," alifafanua Mtatiro.

## TPHPA yarudisha furaha wakulima Manyara

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA), imedhibiti ndege wasumbufu milioni tano waharibifu wa mazao na kuokoa hekari 1,000 katika Kata ya Kisangaji mkoani Manyara.

Mtaalamu wa Kudhibiti Visumbufu vya Mimea kutoka TPHPA, Gladman Mbukonyi, alitoa taarifa hiyo wakati wa kudhibiti ndege hao waharibifu wa mpunga, akibainisha kuwa mamlaka hiyo ina mpango wa kuanzisha mfumo wa utabiri ili kuwawezesha kufahamu tatizo la mlipuko lilipo kwa wakati.

Alisema idadi ya ndege waliodhibitiwa katika kata hiyo ina uwezo wa kuharibu tani 50 za mazao kwa siku.

"Ndege hawo wangeachwa wangeweza kuharibu zaidi ya hekari 1,000 kwa muda mchache na kukwamisha jitihada za wakulima. Mikakati ya TPHPA ni kuhakikisha mkulima anafurahia kushiriki katika kilimo, tutatoa ushirikiano pale watakapotuhitaji," alisema.

Kaimu Meneja wa Usimamizi wa Visumbufu vya Mlipuko kutoka TPHPA, Godlove Kirimbo, alisema katika kukabiliana na visumbufu hivyo wamenunua ndege zisizo na rubani (drone) za kutambua vilipo visumbufu na kupuliza dawa ili visilete madhara kwa wakulima.

"TPHPA kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) na Umoja wa Ulaya (EU), tumenunua drone ambazo zinatambua vilipo visumbufu na kunyunyiza dawa, hivyo mazao ya wakulima yatakuwa salama," alisema.

Vile vile, alisema wanatarajia kununua ndege mpya itakayosaidia kupambana na visumbufu hivyo na kubwa zaidi kwenye mipango ya mamlaka hiyo ni kuanzisha mfumo wa utabiri utakaowezesha kutambua na kufika kwa wakati kudhibiti visumbufu hivyo.

Alisema mfumo huo utashirikisha wadau wote walioko kwenye mnyororo wa kilimo, waweze kupata taarifa kwa wakati na kuchukua hatua.

"Natoa wito kwa wakulima kushirikiana na halmashauri kutoa taarifa ili tuweze kukabiliana na visumbufu," alisema.

Kaimu Meneja wa TPHPA Kanda ya Kaskazini, Juma Mwinyimkuu, alisema visumbufu vinachangia kupungua kwa tija ya uzalishaji kwa wakulima, hivyo watavidhibiti ili kumwinua mkulima.

Alisema TPHPA kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo itadhibiti visumbufu vyote ili kuongeza tija ya uzalishaji na kukuza uchumi.

"Jitihada zetu za kudhibiti visumbufu kama ndege, zinaenda kuifanya Tanzania kutekeleza Malengo Endelevu ya Dunia (SDGs) lengo namba moja la kuondoa umaskini na lengo la kuondoa njaa," alisema.

Mtaalamu wa Viuatilifu na Afya ya Mimea Halmashauri ya Babati, Kanas Sulu, alisema operesheni hiyo iliyotekelezwa na TPHPA itawezesha wakulima kupata mavuno yatakayowaingizia kipato wao na halmashauri.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Shaurimoyo, Florian Ngowi, alisema wakulima wa mpunga na mazao mengine wamezoea kutumia udongo kufukuza visumbufu vya mazao, ujio wa ndege hizo utawawezesha kujikita na shughuli zingine za kiuchumi.

Mkulima wa Mpunga, Mariam Gadiel, alisema matumizi ya ndege za kufukuza na kuua ndege waharibifu umewapunguzia gharama katika kilimo, akibainisha kuwa awali walikuwa wanakodisha vijana kwa ajili ya kufukuza ndege na kulazimika kuwalipa fedha hadi wakati wa kuvuna.



Mkurugenzi wa Uzalishaji kutoka Wakala wa Taifa wa Uzalishaji na Uendelezaji wa Mbegu za Kilimo (ASA), Dk. Justin Ringo, akitoa maelezo kwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Ummy Nderiananga, kuhusu shughuli zinazofanywa katika mashine za kuchakata mbegu, alipokuwa kwenye ziara ya kukagua utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi AFDP inayoratibiwa na ofisi yake mkoani Morogoro. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

AGIZO LA GWAJIMA

## Washereheshaji wajipanga kutoa elimu kuzuia watoto kutumika kucheza usiku

**Na Jenifer Gilla**

WASHEREHESHAJI, waongoza muziki (DJ) na wasimamizi wa kumbi za sherehe jijini Dar es Salaam, wamefunguka walivyojipanga kuzuia ushiriki wa watoto sherehe za usiku kwa kutoa elimu.

Uamuzi huo umekuja siku chache baada ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, kuwataka washereheshaji kuzingatia Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2009 iliyorekebishwa mwaka 2019, wanapotekeleza majukumu yao ili kumlinda mtoto dhidi ya vitendo visivyo na maadili.

Agizo hilo alilitoa Septemba 12, mwaka huu, siku chache baada ya kukerwa na video iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii inayowaonyesha watoto wawili wa kike wakicheza wimbo usio na maudhui mazuri kwa staili isiyo na maadili kwa umri wao katika sherehe iliyofanyika usiku kinyume na kifungu namba 158 (1) (B).

Akifafanua kifungu hicho, Waziri Dk. Doroth alisema kinakataza watoto kutumiwa kwenye sherehe za harusi, maonyesho ya mavazi au shughuli nyingine zinazofanyika usiku na kuzikumbusha familia na jamii kuzingatia malezi ya watoto kwa kufuata sheria hiyo ili kuwalinda.

Dk. Gwajima aliwaagiza wasanii wakiwamo wanamuziki na waigizaji kuandaa kazi zenye maudhui yenye kulinda maadili na kumlinda mtoto huku akiwaelekeza watumiaji wa mitandao ya kijamii kutekeleza Sheria ya Mtoto.

Katika ukurasa wake wa Instagram wa mshereheshaji Nabihundu Nsena, maarufu MC Nsemna, aliweka video fupi akiwaelimisha waliohudhuria sherehe aliyokuwa anaongoza kutii sheria hiyo kwa kutoambatana na watoto walio chini ya umri wa miaka 18 kwenye sherehe ya aina yoyote ya usiku wala kwenda nao katika maeneo wanayouza vinywaji vyenye vileo.

"Kwa hiyo mtu yeyote atakayeshikwa akiwa anatumia watoto kujinufaisha kwa kitu chochote au kuwa nao kwenye sherehe atahukumiwa kwa mujibu wa vifungu mbalimbali vya sheria ya mtoto. Kwa hiyo nimesimama hapa nikiwakumbusha Watanzania wenzangu tuwe makini sana katika hilo," alisema.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii, mshereheshaji Amadi Gwaje, maarufu MC Gwaje, alisema anatumia nguvu yake kubwa ya ushawishi aliyonayo kwa jamii kutoa elimu ya kutekelezaji wa sheria hiyo katika shughuli, kama waziri alivyoliagiza ili kujenga vizazi vya kesho vyenye maadili yanayokubalika.

Alisema elimu hiyo anaitoa kuanzia kwenye vikao vya shughuli husika pamoja na kukataa tukio lolote linalohusisha ushiriki wa watoto ikiwamo kucheza au maigizo katika sherehe za usiku.

"Kwa kuwa MC tunashiriki katika vikao vya harusi na kupanga ratiba za sherehe, tuna nafasi kubwa ya kuzuia ushiriki wa watoto kwa kukataa ajenda zitazohusu ushiriki wa watoto katika sherehe hizo, hicho ndicho nitakachofanya," alisema MC Gwaje.

Kapewa Rajabu, maarufu MC Kapewa, alisema mara zote akiwa anahudumu shughuli zinazohusu watu wazima na kufanyika usiku, haruhusu watoto kuingia kwa kuwa anaelewa maudhui yanatayofanyika hayawajengi bali yanawabomoa.

"Mimi mwenyewe ni mama, nina mtoto mdogo wa kike ambaye nisingetamani ajifunze mambo yanayofanyika kwenye 'kitchen part' kwa sababu makubwa kuliko umri wao na watoto hawana uwezo wa kuchuja mambo," alisema.

Meneja wa ukumbi wa sherehe, John Joseph, alisema atashirikiana na mwenyekiti wa kamati ya harusi pamoja na viongozi wa mtaa kudhibiti uingizaji watoto katika ukumbi wake nyakati za usiku.

Alisema wateja wanapata maelekezo ya kufuata sheria ikiwamo za mtoto tangu wanapopewa kibali cha kuendesha sherehe hizo, lakini baadhi yao wanaamua kukaidi na kwenda na watoto.

Alisema watoto pia wanaathiriwa na hali ya hewa ya viyoyozi, sauti zilizopitiliza na maradhi yanayoambukizwa kwa hewa ikiwamo kifua kikuu na Uviko-19.

Alishauri viongozi kwa kushirikiana na polisi jamii kufanya doria katika kumbi za sherehe zilipo mitaani mwao kukagua na kuchukua hatua watakapobaini sheria hiyo imevunjwa.


KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
ARUSHA

UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI

SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 19 LA MWAKA 2023

MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MICHAEL NGALEKU SHIRIMA-MAREHEMU

NA

CHRISTIAN CHARLES SHIRIMA- MWOMBAJI

TAARIFA YA KAWAIDA
(KANUNI YA 25)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia maombi haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa barua za usimamizi waemirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 7 Mwezi Novemba,2023.

Imewasilishwa Arusha leo tarehe 11 Mwezi Septemba,mwaka wa 2023

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
ARUSHA

RIPOTI MAALUM

# Hatari kwa wanaotumia Fragyl kuzuia ujauzito

**Na Christina Mwakangale**

MATUMIZI ya kiwango kikubwa ya dawa ya Fragyl (metronidazole) ni hatari kiafya, lakini imebainika baadhi ya mabinti wanazitumia kama njia mojawapo ya kupanga uzazi.

Madaktari bingwa wanaonya mtu anayemeza kiwango cha dawa hizo, yuko hatarini kuathiri uoni, utendaji kazi wa ubongo, kujenga usugu wa dawa na kuleta upinzani wa matibabu, lakini imebaini baadhi ya mabinti wanameza hadi vidonge 12 vya Fragul kwa siku ili kuzuia kupata ujauzito.

Katika udadisi wake jijini Dar es Salaam, mwandishi wa habari hizi amebaini mabinti, hususan wanachuo wanaoishi jirani vyuo vya elimu, ni miongoni mwa wanunuzi na watumiaji wa dawa hiyo, huku baadhi yao wakijipangia ratiba ya kuzimeza, baadhi wakimeza hadi vidonge 12 kwa siku.

Moja ya sababu zinazotajwa na mabinti hao waliozungumza na mwandishi, ni upatikanaji wake kuwa wa uhakika na huuzwa bei rahisi wanayoimudu.

Vilevile, baadhi ya mabinti hao wanadai Fragyl ni njia rahisi zaidi ya uzazi wa mpango kulinganishwa na njia zinginezo kama vile vipandikizi, sindano na vidonge vya uzazi wa mpango.

"Binafsi ninameza Fragyl mara moja moja ili kuzuia mimba. Kuna zile P2 ambazo zinafanya kazi ya kuzuia mimba, ila inauzwa ghali kwangu. Mimi mwanafunzi, sina fedha nyingi. Fragyl ukiwa na buku (Sh. 1,000) hata 500 unapata vidonge," anasema Adeline (si jina halisi).

Mwanafunzi huyo wa mwaka wa kwanza anayesomea kozi ya Utawala wa Biashara katika Chuo Kikuu cha Kimataifa Kampala (KIU) Dar es Salaam, anasema matumizi ya Fragyl kwake hayaepukiki, akitaja ni njia rahisi kwake kukabiliana na ujauzito.

Vilevile, mwandishi alizungumza na wanafunzi wanaosoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na vyuo vingine vya jijini wanaoishi maeneo ya Gongo la Mboto, Hosteli za Mabibo na Mwenge Mpakani.

Katika udadisi wake, mwandishi amebaini kwamba katika maduka ya dawa yaliyoko katika maeneo hayo, Fragyl ni miongoni mwa dawa zenye soko kubwa, wateja wakuu wakiwa ni mabinti wanavyuo.

"Ugonjwa ni siri ya mteja anayekuja kununua dawa, ameandikiwa na daktari au la. Mimi ninamwuzia kwa sababu hii ni biashara. Na wapo wateja wengi ambao wananunua dawa tofauti kwa dozi ya siku moja au tano, inategemeana na fedha zake.

"Fragyl au dawa yenye 'metronidazole' inauzika sana, sijui kwanini. Wanaonunua ni wa rika tofauti wakiwamo wasichana. Hapa ni jirani na chuo, wengine wananunua P2. Sasa utaanzaje kumhoji mteja kwanini ananunua dawa hii? Ni ngumu. Ninawaandikia matumizi yake, kama inavyoelekezwa ila akiwa huko akibadili matumizi, siwezi kufahamu," anasema Mwajuma Chaula.

Mwajuma ni mwuzaji wa duka la dawa lililoko Gongo la Mboto, jijini Dar es Salaam. Anasema miongoni mwa dawa ambazo kasi ya mauzo imeongezeka ni 'metronidazole' (Fragyl), ambayo dozi moja huuzwa kati ya Sh. 1,000 hadi 1,500.

**HATARI KIAFYA**

Daktari Bingwa wa Uzazi kutoka Idara ya Uzazi Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala, Mugalu Kitandu, anasema matumizi ya dawa aina hiyo kwa kiwango kikubwa ni hatari kwa afya.

Dk. Kitandu anafafanua kuwa matumizi ya dawa hiyo kwa kiwango kikubwa yamedhihirisha kwa wanyama kama panya, kuwa chanzo cha vivimbe vinavyohusishwa na saratani kama vile saratani ya matiti. Pia husababisha sumu na ganzi mwilini kutokana na uharibifu wa neva.

"Kuna utafiti ulifanyika kwa wanachuo wa UDOM (Chuo Kikuu cha Dodoma). Wengi walikubali kuwa wanakunywa karibia vidonge 12 kwa siku. Dozi kubwa namna hiyo hazitakiwi kwa binadamu. Dozi ya kawaida ya Fragyl ni vidonge sita kwa siku," afafanua bingwa huyo.

UTAFITI VYUONI

Utafiti uliopewa jina 'Metronidazole (Fragyl), Matumizi ya Dharura Yanayohusisha Wanafunzi Wanawake vyuoni Mkoa wa Dodoma, Tanzania; Utafiti Kimaelezo na Mtambuka', umefanywa katika vyuo vikuu vitatu vilivyoko Mkoa wa Dodoma.

Utafiti huo ulikusanya taarifa kwa wahojiwa 470, wote ni wanawake walio katika umri wa kuzaa, yaani miaka 18 hadi 45 kwa kipindi cha kuanzia Mei hadi Julai, 2021. Ulitolewa Januari mwaka huu (2023).

Kati ya wahojiwa 470 waliohusishwa na utafiti, 446 sawa na asilimia 94 hawajaolewa au wamo katika uhusiano usio rasmi na 24 pekee wamo katika ndoa.

Lengo la utafiti huo ambao mwandishi wa habari hizi ameona ripoti yake, ni kubaini ongezeko la idadi kubwa na wanavyuo kutumia bila mpangilio dawa ya metronidale maarufu kwa jina la kibiashara la Fragyl.

Ilibainika kuwa baadhi wananunua toka maduka ya dawa kama njia ya uzazi wa mpango kinyume cha matumizi ya dawa hiyo ya antibaiotiki.

Utafiti ulifanywa katika taasisi za elimu ya juu tatu zilizoko manispaa ya Dodoma, mkoani Dodoma ambavyo ni Chuo Kikuu cha St. John, Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na UDOM Ndaki ya Sayansi ya Jamii.

Matokeo yameonesha wahojiwa 169 walisema wanatumia Fragyl kama njia ya uzazi wa mpango; 139 wanatumia P2 kama njia ya uzazi wa mpango na 271 hawajawahi kutumia njia yoyote ya uzazi.

Vilevile, wanachuo 345 kati ya waliohojiwa, walisema wamewahi kusikia mtu akiitumia dawa hiyo kama njia ya kupanga uzazi. Utafiti pia ulibaini dawa hiyo kwa wanayoitumia hunywa dozi kubwa kwa kipindi kifupi ndani ya saa 24 huku 42 wakionesha walipata dawa hiyo duka la dawa; asilimia 39 hospitalini na asilimia 17 wakiipata dawa hiyo kutoka kwa marafiki.

Kati ya waliohojiwa, asilimia 71 ya wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 21 walijibu wanaitumia Fragyl kama njia ya dharura ya uzazi wa mpango; miaka 22 hadi 25 kwa asilimia 90 wanaitumia dawa hiyo na alio na miaka 26 hadi 29 kwa asilimia nane walisema wanaitumia dawa hiyo.

Watafiti wanasema sababu ya matumizi ya dawa hiyo kwa mujibu wa wahojiwa, kwa asilimia 59 walisema ni rahisi kuipata, asilimia mbili walisema haina kiwango kikubwa cha hatari kama mbinu nyingine za kupanga uzazi, asilimia 33 wanaona aibu kuulizia dawa aina nyingine ya rasmi ya uzazi wa mpango huku asilimia sita wakidai inauzwa kwa bei rahisi.

**NINI KIFANYIKE**

Anaporejeshwa Daktari Bingwa wa Uzazi, Dk. Kitandu, anasema elimu inapaswa kutolewa kwa vijana kuhusu mabadiliko ya mwili na namna ya kuepukana na ngono ambayo ni chanzo cha matumizi holela ya dawa.

Anasema athari za matumizi holela ya dawa hizo ni kuharibika kwa mimba na hatari kwa afya ya binadamu.

"Mbali na matumizi ya P2 kuwa makubwa kama ambavyo hata Waziri wa Afya ameshakemea, matumizi ya dawa hiyo ni maalum kwa dharura tu. Sasa hivi wasichana wanatumia dawa yenye 'metronodazole' wakidai baada au kabla ya tendo ni kinga ya mimba.

"Kuna haja ya kuongeza wigo wa elimu ya afya ya uzazi na taarifa sahihi kuhusu afya uzazi, ili vijana hawa wajue watumie ipi. Kiuhalisia mabinti walioko vyuoni, hata shuleni hasa shule za sekondari wanajihusisha na ngono. Matokeo yake ni mimba, utoaji mimba holela na kuhatarisha uhai.

"Fragyl inazuia kujipandikiza kwa 'embryo' (mimba). Kwa asilimia 70 inaweza kusababisha mimba kutoka, yai likisharutubishwa 'metronidazole' inazuia lisikae kwenye ukuta wa kizazi.

"Lakini dozi kubwa ya dawa hii inahusishwa na vivimbe, unaweza kupata saratani. Haya majibu yalitoka kwenye utafiti wa wanyama, kwa sababu dozi kubwa namna hiyo hazitakiwi kutumiwa na binadamu na hakuna utafiti uliothibitisha kwa binadamu, lakini muhimu kujihadhari," anahadharisha.

Bingwa huyo anabainisha kwamba dawa hiyo ya antibaiotiki ikitumika isivyo, madhara yake ni kujenga usugu wa dawa. Badala ya kutibu ugonjwa husika kulingana na ushauri wa kitaalamu, aliyetumia dawa hizo kwa kiwango kikubwa hawezi kutibiwa kwa dawa za kawaida kwa kuwa mwili wake umejenga usugu kwa dawa.

Anasema changamoto ni kubwa kwa sababu za maadili ya kiafya, hakuna utafiti uliobainisha ama kuruhusu Fragyl kutumika mara mbili ya dozi inayotakiwa.

"Antibaiotiki inakuwa sugu mwilini, maana yake vidudu vinabadilika, vinazoea dawa, vinakuwa haviwezi tena kuuliwa na hiyo dawa, tofauti na mwanzo kwa sababu vimepewa hiyo dawa kinyume cha matumizi.

"Hii ndio vita kubwa sasa hivi kitabibu, kwa sababu dawa zilizokuwa zinatibu baadhi ya magonjwa, haziwezi tena siku hizi. Chanzo ni tulizitumia vibaya. Kunywa vidonge 12 siku moja ni hatari. Kawaida ni vidonge sita ambavyo ni viwili mara tatu kwa siku," anafafanua.

**AFYA UZAZI**

Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zina kiwango cha juu cha mimba na ndoa za utotoni, asilimia 27 ya wasichana nchini walikwishazaa katika umri wa miaka 15 hadi 19 kufikia mwaka 2016 kwa mujibu wa Takwimu za Kitaifa za Utafiti wa Hali ya Afya (TDHS).

Ofisa Programu Mkuu kutoka Mtandao unaojihusisha na Ukimwi, Huduma za Afya Afrika Mashariki (EANNASO), Denis Bwana, anasema asilimia 22 ya wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 19 wamewahi kubeba ujauzito na asilimia 16 ya wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 19 wamewahi kujifungua watoto hai.

Pia anabainisha kuwa asilimia mbili ya wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 19 nchini, walikuwa na ujauzito ulioharibika/mtoto mfu/mimba kutoka huku asilimia sita ya wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 19 kwa sasa ni wajawazito.

Ofisa Mwandamizi wa Afya wa Shirika la Pathfinder, Dk. Samuel Kikaro, anasema dhana iliyoko miongoni mwa vijana hasa walioko masomoni ni kuogopa mimba, hivyo baadhi hudiliki kutumia mbinu tofauti kuzuia, ikiwamo zisizo za kitaalamu kama vile kutumia dawa kiholela.

"Hivi sasa mabinti wanaogopa mimba, yaani watoto wanaogopa mimba kuliko Ukimwi. Kwenye njia za uzazi wa mpango kuna minong'ono mingi, imani potofu, tamaduni za Kiafrika kwamba zina athari, lakini ukweli ni kwamba vijana wetu tena wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 24, baadhi wanashiriki ngono. Tusidanganyane, tutafute njia ya kuwaepusha na matokeo ya ngono.

"Ipo haja ya kuongeza elimu ya afya ya uzazi, kwa sababu takwimu za kitabibu zinasema mimba chini ya miaka 20 ni hatarishi, pia asilimia 25 ya walio katika umri wa kuzaa nchini, wanahitaji huduma ya afya ya uzazi ila hawafikiwi na huduma," anasema Dk. Kikaro.

Anabainisha kuwa kiwango cha utoaji mimba kwa siku ni mimba 36 katika kila wanawake 1,000 walio kwenye umri wa kuzaa nchini. Kati yao, wapo ambao hupoteza maisha.

"Kuzaa chini ya miaka 20 ni hatari kwa wasichana na tuna asilimia 54 ya vijana wote nchini walio chini ya miaka 20, idadi hii ni kubwa isipoelimishwa kuhusu afya ya uzazi na uzazi wa mpango.

"Ikumbukwe uzazi usio wa mpango unaongeza kiwango cha utegemezi, nchini utegemezi ni asilimia 80 na asilimia 19 pekee ndio wazalishaji," anasema Dk. Kikaro.





Wataalamu wa upasuaji wa moyo kwa watoto kutoka Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) na mwenzao kutoka Chuo Kikuu cha Jagiellonian nchini Poland, Prof. Tomasz Mroczek, wakifanya upasuaji wa kurekebisha mishipa ya damu ya moyo ambayo haijakaa katika mpangilio wake wakati wa kambi maalumu ya siku tano ya matibabu ya magonjwa ya moyo kwa watoto iliyofanyika JKCI. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watetezi jinsia wataka sera taulo za kike zigawiwe bure shuleni

**Na Salome Kitomari**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP) umeitaka serikali kuja na sera itakayowezesha taulo za kike kugawiwa bure katika shule za msingi na sekondari, ili kupunguza kero wanayokutana nayo watoto wa kike.

Vilevile, mtandao huo umesema kuwa ili kuboresha utendaji katika serikali za mitaa ni muhimu kuwa na mabadiliko ya kisera ili madiwani walipwe na hazina moja kwa moja.

Akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni kuhusu maandalizi ya tamasha la kimataifa la jinsia litakalowaleta pamoja zaidi ya watu 1,500, Mwenzeshaji kutoka TGNP, Deo Temba, alisema ni muhimu serikali ikawezesha jambo hilo kwa kuwa linawezekana badala ya kuweka namna ya kupata kodi.

"Tunapendekeza taulo za kike zigawanye bure ili hata mtoto wa maskini asiwe na kikwazo cha kwenda shuleni, ni jambo linalowezekana kabisa, kwa sasa limekuwa jambo la kibiashara na wale wanaojitolea kupitia kampeni mbalimbali," alisema.

Moja ya taasisi inayofanya kampeni ya kukusanya taulo za kike kutoka kwa Watanzania ni Kituo cha East Africa TV na Radio ambao wana lengo la kukusanya taulo 10,000.

Kuhusu madiwani, Temba alisema maeneo mengi waliyotembelea walibaini kuna changamoto kubwa kwa viongozi hao kwa kuwa malipo yao yanasuasua.

"Tunamkumbusha Rais Samia Suluhu Hassan ile nia yake kwamba madiwani walipwe kupitia Hazina. Hii itaondoa kero na mzigo mkubwa kwa halmashauri," alisema Temba.

Alisema wananchi wameshiriki mchakato wa bajeti kuanzia ngazi ya chini hadi juu, ikiwamo kuweka vipaumbele vyao, jambo lililosaidia kuwa na bajeti jumuishi hasa kwenye ngazi ya halmashauri.

"TGNP imechukua wananchi wa ngazi ya kitongoji kwenda kuonana na wabunge, makatibu wakuu na mawaziri, kisha wakatatuliwa mambo yao kwa urahisi kabisa na sauti zao kusikika kwa urahisi," alisema.

Temba alisema hatua nyingine ni utengaji wa bajeti kwa kuzingatia usawa kwa makundi yote kwenye jamii kwa kujua imetolewa kiasi gani, imetumikaje na kwenye miradi gani ambayo ni ya jamii.

Ofisa Habari wa TGNP, Monica John, alisema shirika hilo linafikisha miaka 30 tangu kuanzishwa kwake huku kukiwa na mafanikio lukuki ikiwamo kuongoza vuguvugu la ukombozi wa wanawake na mtoto wa kike, pamoja na kushawishi wanawake wengi kugombea nafasi za uongozi.

Alisema tamasha hilo litakalofanyika Novemba mwaka huu litawaleta wanaharakati kutoka sehemu mbalimbali duniani kwa ajili ya kubadilishana ujuzi, kusherehekea mafanikio na kuangalia changamoto zilizoko katika jamii.

Alisema tamasha litakuwa na kaulimbiu ya 'Miaka 30 ya TGNP na Takwa la Ukombozi wa Wanawake' huku kukiwa na mada ndogo za 'Nyayo zetu na urithi wetu' na 'simulizi za kuleta mabadiliko na mikakati'.

Kwa mujibu wa Monica, mada nyingine ni ubunifu na teknolojia, kuwajengea uwezo vijana kwenye uongozi, mjadala wa viongozi wakongwe na vijana, madiwani wa halmashauri, maofisa maendeleo ya jamii na watu waliopitia changamoto mbalimbali katika jamii.

Alisema kwa miaka 30, TGNP inajivunia mengi ikiwamo mabadiliko ya sheria mbalimbali ikiwamo Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ambayo inawalinda wasichana na wanawake dhidi ya kulazimishwa kufanya ngono na matukio mengine ya ukatili wa kijinsia.

Alisema sheria inatoa adhabu kali ikiwamo kifungo cha miaka 30 kwa kuvunja haki ya kusema hapana na za kimapenzi za wanawake.

Mafanikio mengine ni kuwa na bajeti yenye jicho la jinsia kitaifa huku kwenye ngazi ya halmashauri ni kutenga bajeti za kijinsia.

Monica alisema tangu kuanza kwa tamasha mwaka 2001, zaidi ya watu 35,000 wameshiriki na la mwaka huu linawaleta wadau wa mataifa mbalimbali ambao watatoa simulizi, mabadiliko ya kisera na sheria, safari ya miaka 30 ya vuguvugu la maendeleo ya wanawake na wale wa chini kabisa kukutana na watu wa ngazi za juu za uongozi.

# Biteko: Serikali itaendelea kushirikiana na migodi, mpeni ushirikiano Mavunde

**Na Mwandishi Wetu, GEITA**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ameahidi Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kuendelea kuungwa mkono na serikali ili kuifanya sekta ya madini kukua na Watanzania wafaidika na rasilimali zao.

Dk. Biteko pia ametoa rai kwa uongozi wa kampuni hiyo kumpa ushirikiano wa kutosha Waziri mpya wa Madini, Anthony Mavunde ili atimize malengo aliyojiwekea, ikizingatiwa huo ndio mgodi mkubwa wa madini ya dhahabu kuliko yote nchini.

Alitoa kauli hiyo juzi alipotembelea Banda la GGML katika Maonesho ya Sita ya Teknolojia ya Madini Geita, pia katika hotuba yake ya kufungua maonesho hayo yanayoendelea katika Viwanja vya Bombambili -EPZA Geita mjini hapa.

Akiwa katika banda la mgodi huo, Dk. Biteko alisema kampuni hiyo imekuwa mshirika mkubwa wa serikali na anafarijika kwa kuwa mwekezaji hai kupitia Mpango wa Uwajibikaji kwa Jamii (CSR).

"Hata Mkuu wa Mkoa wa Geita (Martin Shigela) amesema ninyi ndio wadhamini wakuu wa maonesho haya. Kwahiyo, tunawapongeza sana," alisema.

Aliongeza kuwa kuwa sasa sekta hiyo ina waziri mpya, yeye inawezekana alikuwa waziri mpole kidogo, lakini amekuja Waziri Mavunde ambaye ni mkali. Apewe ushirikiano.

"Mpeni ushirikiano ili sekta hii tuitoe izidi kukua kwa sababu mgodi wa GGML ndio mfano wa migodi yote nchini. Kwahiyo, tusipofanya vizuri Geita na migodi mingine haitafanya vizuri. Tukifanya vizuri, migodi mingine itafanya vizuri. Lakini ninawapongeza sana," alisema Dk. Biteko.

Wakati wa ufunguzi rasmi wa maonesho hayo juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Terry Strong, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake za kuboresha mazingira rafiki kwa wawekezaji nchini.

Strong alisema jitihada Rais Samia kufuatilia kwa umakini sekta binafsi na sekta ya madini na kutatua changamoto zake, zimeibua matumaini katika eneo hilo lenye wadau wengi.

"GGML inaweza kuwa mfano wa kuigwa kutokana na ari hii mpya, baada ya kupata ushirikiano wa kutosha kutoka serikalini. Mathalani katika utekelezaji wa sheria mpya ya madini," alisema.

Alibainisha kuwa sheria hiyo imetoa mwongozo wa usimamizi wa sekta ya madini kuhusu masuala ya kodi, malipo ya mrabaha na matumizi ya fedha za CSR, huku pia ikisisitiza ujumuishaji wa uchumi wa ndani.

"Tunafarijika kusema kuwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, GGML imeshirikiana kwa kiasi kikubwa na Serikali ya mkoa wa Geita, kwa kutenga zaidi ya Sh. bilioni 46 kupitia CSR.

"Fedha hizi zimesaidia kutekeleza miradi kadhaa inayolenga jamii ikiwamo ujenzi wa soko la kisasa na vituo vya huduma ya afya ikiwamo miundombinu ya elimu inayolenga mahitaji ya ndani," alisema.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wachezaji Ligi Kuu Bara jilindeni wenyewe, msitegemee marefa

**NI** msimu mpya wa Ligi Kuu Bara 2023/24, ambapo ligi hiyo inayoshirikisha timu 16, kila moja ikiwa imecheza mechi tatu na Yanga ikiwa kileleni kwa tofauti ya mabao kutokana na kulingana pointi na Simba na Azam FC, kila moja ikikusanya alama tisa.

Hata hivyo, kama ilivyokuwa msimu uliopita kwa waamuzi wengi kuadhibiwa kwa kufungiwa na Kamati ya Waamuzi ya TFF kutokana na kushindwa kuchezesha kwa haki, changamoto hiyo tena imeanza kujitokeza baadhi yao kuanza kuzifinyanga kanuni.

Kilio cha waamuzi kimekuwa kikubwa kila msimu, na hilo halina kificho kwani hata kwenye michuano mikubwa ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na lile la Dunia (Fifa), ni nadra kuona waamuzi kutoka Tanzania wakipangiwa kwenda kuamua mchezo.

Ingawa kwa msimu huu bado hapajawa na makosa mengi hususan ya timu kulalamika kwa kutotendewa haki hadi kuwa chanzo cha kupoteza mchezo, lakini waamuzi wanaonekana kutokuwa makini kwa baadhi ya maamuzi yao hususan suala la rafu.

Waamuzi wengi wanashindwa kutafsiri sheria hususan suala la rafu mbaya zinazoweza kuhatarisha afya za wachezaji wenzao uwanjani, hivyo kushindwa kutoa adhabu ya kadi jambo ambalo huwafanya wanaofanya makosa hayo kuona ni ya kawaida tu.

Mfano ni rafu mbaya aliyochezewa beki wa Yanga, Joyce Lomalisa na Hashimu Manyanya wa Namungo FC kwenye mchezo uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi Jumatano iliyopita, lakini mwamuzi Emmanuel Mwandembwa aliishia kutoa kadi ya njano.

Bila kupepesa, kwa tukio lile lilistahili kadi nyekundu, lakini cha kushangaza, Mwandembwa hakufanya hivyo, hii inawafanya wachezaji kuona hiyo ni rafu ya kawaida hivyo kuendelea kufanya makosa mengine madogo ya kadi ya njano ambayo mara nyingi baadhi ya waamuzi wanayavumilia.

Kosa kama hilo si kwa Mwandembwa pekee, bali yapo mengi yanayofanana na hayo ambayo yamekuwa yakifanyika na waamuzi wengine katika michezo ya Ligi Kuu na hata ile ya Championship na First League hapa nchini, hivyo marefa wanapaswa kubadilika sasa kwa kufuata kanuni zinazoongoza mchezo huo pendwa duniani.

Tunatambua kadi ya njano ni kwa ajili ya kutoa onyo na kumkumbusha mchezaji wajibu wake wa kulinda afya ya mchezaji mwenzake kwa kucheza mchezo wa kiungwana (fair play) wakati wote, na kumfanya atambue kosa lingine katika mchezo huo litamfanya atolewe kwa kadi ya pili ya njano inayoambatana na nyekundu ama nyekundu moja kwa moja.

Hivyo, kadi ya njano inapotolewa kwa mchezaji humfanya kucheza kwa nidhamu zaidi, jambo ambalo ndicho wapenzi wa soka wanachotaka kukiona uwanjani lakini pia ni kwa manufaa ya kulinda afya ya wenzake. Tunawakumbusha waamuzi kutovumilia rafu na kamwe wasione ni dhambi kutoa kadi za njano ama nyekundu pale inapostahili, kwani kwa kufanya hivyo kunaongeza nidhamu kwa wachezaji uwanjani na kuufanya mchezo kuwa burudani ambayo ndiyo mashabiki na wapenzi wa mpira wanayotaka kuishuhudia.

Tunachotaka kukiona ni kadi za njano na nyekundu zinatolewa pale inapostahili na si waamuzi kusubiri hadi mchezaji aumizwe na kushindwa kuendelea na mchezo ndipo wachukue hatua hizo.

Lakini pia wachezaji hawana budi kuona umuhimu wa kulindana afya zao wenyewe uwanjani kwa kucheza soka la kiungwana badala kusubiri waamuzi ambao baadhi wamekuwa wakizifinyanga kanuni za soka pengine kwa kutojua au kwa masilahi yao ama dhamira zao ovu wenyewe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba, Yanga zisaidiwe kimataifa kwa kucheza ligi, si kuziahirishia

Na Adam Fungamwango

**BADO** kuna baadhi ya viongozi wa soka nchini wanaamini kuwa ukiziahirishia timu zinazocheza kimataifa mechi za Ligi Kuu unakuwa unazisaidia sana ili zifanye vema.

Huko nyuma wengine waliamini hivyo, lakini taratibu hiyo inaanza kuondoka vichwani mwa baadhi ya mashabiki wa soka nchini.

Nadhani kuna baadhi ya viongozi kwenye Bodi ya Ligi na hata klabu zinazoshiriki wanaendelea kuamini timu inapokaa wiki mbili bila kucheza kwa ajili ya kujiandaa na mechi za kimataifa kuna uwezekano mkubwa wa kushinda mechi hiyo.

Klabu ya Simba hivi karibuni iliomba mechi dhidi ya Coastal Union kwa sababu ya kuwaweka fiti wachezaji wake kuelekea kwenye mechi dhidi ya Power Dynamos, lakini Bodi ya Ligi (TPLB), ilikataa.

Viongozi wa Simba waliamini kuwa mechi hiyo ingeendelea kuwafanya wachezaji wake waendelee kuwa na utimamu wa mwili na wa mechi kuelekea mchezo wao wa kimataifa.

Nadhani viongozi wa Simba walikuwa wamejifunza baada ya kuomba kuahirishwa mechi zao za ligi wakati ilipokuwa ikijiandaa kucheza dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini katika mechi yao ya kwanza iliyopigwa Sauzi, Mei 15, 2021.

> **Simba ilikaa kiasi cha wiki mbili hivi bila kucheza mechi yoyote ya ligi, kilichowakuta ni kwamba ilifungwa mabao 4-0, kabla ya kushinda 3-0 katika mchezo wa marudiano uliochezwa wiki moja tu baada ya mechi hiyo.**

Simba ilikaa kiasi cha wiki mbili hivi bila kucheza mechi yoyote ya ligi, kilichowakuta ni kwamba ilifungwa mabao 4-0, kabla ya kushinda 3-0 katika mchezo wa marudiano uliochezwa wiki moja tu baada ya mechi hiyo.

Ilishinda mabao 3-0 kwa sababu tayari wachezaji wao walikuwa wamepata utimamu wa mwili kutokana na mechi hiyo.

Timu za Simba, Yanga na Singida Fountain Gate, binafsi sikuona sababu ya wiki hii timu hizo kutokuwa na mechi za Ligi Kuu kuelekea katika mechi zao za kimataifa.

Yanga ilicheza mechi yake ya Ligi Kuu Jumatano iliyopita dhidi ya Namungo, Simba ikacheza dhidi ya Coastal Union kesho yake Alhamisi na Singida Fountaine Gate ambayo nayo inashiriki kimataifa ikacheza mechi yake siku hiyo usiku dhidi ya Azam FC.

Hakukuwa na sababu ya Jumamosi na Jumapili au Jumatatu na Jumanne timu hizo kila moja zisicheze mechi moja ya Ligi Kuu kwa ajili ya kuwaweka fiti wachezaji wake.

Kungekuwa na mechi hizo sidhani kama hata klabu zingewaruhusu wachezaji kwenda mapumziko wikiendi iliyomalizika. Baada ya kumaliza mechi za ligi, moja kwa moja zingerudi kambini kujiandaa huku wachezaji wao wakiwa fiti na utimamu wa mwili kwa asilimia 100.

Badala yake nimesikia timu zote mbili ziliruhusu wachezaji wake wakapumzike wikiendi hii kwa sababu hakukuwa na mechi.

Sheria inaruhusu kabisa timu ikicheza mechi Jumatano, Jumamosi kuweza kucheza tena na inayocheza Alhamisi inaweza kucheza Jumapili. Basi walau zingecheza Jumatatu na Jumanne. Hiki kinachofanyika na Bodi ya Ligi sidhani kama kinazisaidia timu hizi badala ya kuzidumaza.

Timu hizi, hasa Simba na Yanga huenda zikatinga hatua ya makundi, Bodi ya Ligi inapaswa ijifunze ni jinsi gani itawafanya wachezaji wake wawe wakakamavu na si legelege.

Na hili litatimia kwa kuwafanya wacheze mechi nyingi mara kwa mara mechi za Ligi Kuu, na wakati mwingine iwe wiki moja kabla ya mechi za kimataifa si kuziahirisha michezo zao za ligi.

# Waziri Mkuu atoa siku 5 kituo kipewe watumishi

**Na Restuta Damian,** MISSENYI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa siku tano kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, kupeleka watumishi wa afya katika kituo cha Afya cha Kakunyu Wilaya ya Missenyi ili kuanza kutoa huduma kwa wananchi baada ya jengo la nje kukamilika.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki baada ya kumaliza kukagua kituo hicho ambacho kimejengwa kwa mapato ya ndani kwa thamani ya Sh. milioni 532 na kukamilisha majengo matano muhimu ya kutolea huduma za wagonjwa.

Aliagiza majengo hayo kuanza kutumika kwa kutibu magonjwa ya kawaida wakati taratibu nyingine za kuleta vifaa tiba, vitendanishi na kujenga majengo ya upasuaji yakikamilishwa na serikali.

Alisema kuwa ndani ya mwezi mmoja serikali itapeleka vifaa vyote vya uchunguzi, lakini huduma za kawaida kwa wagonjwa wa nje haziwezi kusubiri mwezi mmoja kuanza kutolewa badala yake watumishi na thamani za kawaida, dawa na sehemu ya kutunza data vipelekwe katika kituo hicho na wananchi wa magonjwa ya kawaida waanze kupata huduma.

"Hii ni wilaya ya mfano ambayo imetumia fedha za ndani kujenga kituo cha afya ambacho kitaokoa wananchi wanaotembea umbali mrefu kufuata huduma za afya, kuwapo wa kituo hiki ni mkombozi mkubwa kwa wananchi wa vijiji vya hapa Kakunyu, najua wengine walilazimika kwenda Uganda kutafuta tiba, lakini serikali imewasikia na huduma zote mtazipata hapa na kila huduma itapatikana ndani ya mwezi mmoja ujao," alisema Majaliwa.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Fatuma Mwasa, alisema kituo hicho kitakapokamilika kitahudumia vijiji vitatu vya Bugango, Bubale na Kakunyu na wananchi wapatao 28,000 wanatarajiwa kunufaika na kituo hicho.

Aliishukuru serikali kuu kwa kuchangia milioni 90 ambayo imewezesha kujenga nyumba ya watumishi ambayo itawawezesha wafanyakazi kuishi kituoni na kutoa huduma za uhakika.



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, akitoa maelezo kwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (katikati kushoto) kuhusu huduma zinazotolewa na Mfuko huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NSSF yaweka alama maonesho ya madini

## -Juni 2023 imekusanya michango bil. 56/-

**Na Mwandishi,** GEITA

MKURUGENZI Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, amemweleza Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, kuwa NSSF inashiriki Maonesho ya Sita ya Kimataifa ya Teknolojia ya Madini kwa sababu ndio Mfuko pekee wenye jukumu la kuandikisha wanachama kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi wakiwamo wachimbaji wadogo wa madini ili waweze kujiunga na kujiwekea akiba kwa ajili ya maisha yao ya sasa na baadaye.

Mshomba alisema hayo juzi alipokuwa akitoa maelezo kwa Naibu Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko, alipotembelea banda la NSSF katika maonesho hayo yenye kaulimbiu; 'Matumizi ya Teknolojia Sahihi katika Kuinua Wachimbaji Wadogo Kiuchumi na Kuhifadhi Mazingira' yanayoendelea katika viwanja vya EPZA, Bombambili, mkoani Geita. Alisema tangu maonesho hayo yalipoanza mwaka 2018, NSSF imekuwa na mafanikio makubwa kutokana na ushiriki kumechangia ukuaji wa Mfuko na kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2023, walikusanya michango ya Sh. bilioni 56.

"Wakati Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipoingia madarakani, hapa mkoani Geita pekee NSSF ilikuwa inakusanya michango ya Sh. bilioni 29 ambayo ni mara mbili katika kipindi hiki cha miaka miwili na nusu ya uongozi wa Rais, kwa hiyo kwetu sisi ni mafanikio makubwa sana na tunaamini tutaendelea kufanya vizuri zaidi," alisema Mshomba. Aidha, alisema mafanikio ya NSSF kwa ujumla ni mazuri na katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2023, thamani ya michango iliyokusanywa ilikuwa ni ya Sh. trilioni 1.66 na katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2022, thamani ya michango iliyokusanywa ilikuwa Sh. trilioni 1.48.

Mshomba alisema hilo ni ongezeko kubwa na kwamba thamani ya NSSF imeendelea kukua kwa kasi na kwa mujibu wa hesabu zilizokaguliwa mwezi Juni 2022, thamani ya Mfuko ilikuwa Sh. trilioni 6.08 na mpaka kufikia mwezi Juni 2023, imefikia Sh. trilioni 7.6 kwa hesabu zinazoendelea kukaguliwa.


"Huo ni ukuaji mkubwa mno hasa ukizingatia kabla ya hapo na baada ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuingia madarakani, thamani ya Mfuko ilikuwa ni trilioni 4.8 hivyo mafanikio hayo ni kazi kubwa anayofanya Mheshimiwa Rais ya kuvutia wawekezaji," alisema Mshomba.

Alisisitiza kuwa, maonesho hayo ya madini tangu yalipoanza yamekuwa chachu ya ongezeko hilo la wanachama na michango, aliushukuru uongozi wa Mkoa wa Geita chini ya Mkuu wa mkoa huo, Martine Shigela kwa ushirikiano mkubwa wanaowapatia.

Kuhusu matumizi ya TEHAMA, Mshomba alisema NSSF imeweka kipaumbele kikubwa katika matumizi ya TEHAMA ili kurahisisha huduma za wanachama wao jambo ambalo linaendana na kaulimbiu ya maonesho ya madini.

Mshomba alisema NSSF inaendelea kusajili wanachama wapya kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi hususan wachimbaji wadogo ambao ndiyo lengo la Mfuko kushiriki katika maonesho hayo ya madini.

KABWELA Na Fadhili Mohammed



HABARI KITAIFA

# Jumuiya Wazazi CCM yaonya 'uchawa'

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JUMUIYA ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Pwani imeonya wanachama wake kutumia muda mwingi kuwanadi baadhi ya makada wanaotaka kugombea nafasi za uongozi ikiwamo ubunge badala yake wawaambie wananchi miradi iliyotekelezwa na serikali.

Mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Jackson Kituka alitoa onyo hilo jana mjini Kibaha, akiwa na angalizo kwamba hali hiyo imekuwa inashamiri kwa baadhi ya wanachama ambao wamejikita katika mambo hayo aliyoyataja hayana manufaa kwa chama.

Akitoa maelekezo kwa Kamati ya Utekelezaji ya Wilaya ambayo ilikwenda kushiriki mabaraza ya Jumuiya ya Wazazi ngazi ya kata, Kituka alisema ni vyema wanachama wakasisitizwa kujikita kwenye maadili.

"Kumekuwa na tabia ya baadhi ya wanachama kujikita kwenye majukumu ya kuwa chawa na kuanza kupita kwa wanachama wakiwanadi watu wao. Hili halina afya kwa chama chetu na hatuwezi kukubali liendelee.

"Mmezidi sana upambe, kuna wilaya zinaongoza kwa kuwa na watu wa namna hii. Tuweke maslahi ya CCM mbele sio maslahi ya watu binafsi. Kwahiyo, mnapokwenda kwenye kata mkazungumzie kazi nzuri zinazofanywa na serikali na kupinga hili la uchawa," aliagiza.

Katibu wa CCM Mkoa wa Pwani, Marco Mbanga, alisema kuwapo kundi hilo la watu wanaojiita chawa ni kero kubwa kwa chama.

Ni watu wamekuwa wachonganishi.

Alisema: "Kwenye chama kuna watu wema na wabaya na hao wabaya ndio wale chawa. Wengi wao wana njaa, zinawasumbua. Ni wachonganishi, wagombanishi wa watu.

"Sasa niwaonye tu watakaohatarisha ushindi wa chama tutashughulika nao kabla ya madhara kutokea," alisema.

Katibu wa Jumuiya hiyo, Elisante Msuya alielekeza wanachama kufuata kanuni na taratibu za chama ikiwa ni pamoja na kupita kwa wanachama kujiandaa kugombea nafasi za uongozi wakati muda haujafika.

Jumuiya ilishiriki ujenzi wa chumba cha darasa katika Shule ya Msingi Kambarage ya mjini hapa.



Mkurugenzi wa Hazina na Masoko ya Fedha wa Benki ya NBC, Peter Nalitolela (Kushoto) akibadilishana mawazo na baadhi ya viongozi waandamizi wa Jukwaa la Wafanyabiashara wa Afrika Kusini nchini Tanzania wakati wa mkutano wa jukwaa hilo uliofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TBS yazindua tuzo ubora wa bidhaa na huduma

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limefungua mashindano ya tuzo za kitaifa awamu ya nne kwa mwaka 2023 kwa lengo la kuhamasisha ubunifu na uboreshaji bidhaa na huduma.

Wakati wa ufunguzi wa mashindano hayo mwishoni mwa wiki, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Lazaro Msasalaga, alisema wazalishaji na watoa huduma wanahitaji kujijengea utamaduni wa kuzalisha bidhaa zenye ubora na ushindani nchini.

Alisema maombi ya ushiriki wa mashindano hayo yalianza juzi Jumamosi. Yanawasilishwa kwa njia ya nakala ngumu au kielektroniki kwenye ofisi za TBS katika mikoa mbalimbali nchini.

Alisema moja ya hatua zilizochukuliwa na serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara ni kujenga utamaduni wa kuthamini ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini kwa kuanzisha tuzo za kitaifa za ubora kama sehemu ya motisha.

Alisema malengo ya kuanzishwa tuzo hizo ni pamoja na kuwatambua na kuwapongeza watu binafsi waliotoa mchango mkubwa katika kuboresha miundombinu ya ubora.

Alisema mashindano hayo yanalenga kuzitambua pia taasisi zinazofanya vizuri kwenye masuala ya ubora wa bidhaa wakati wa utekelezaji wa shughuli zao za uzalishaji bidhaa au utoaji huduma.

"Matarajio yetu mashindano ya tuzo kwa msimu wa nne kwa mwaka 2023 ambayo tunayazindua leo yatapata hamasa kubwa kutoka kwa wadau wa ubora na hivyo kusababisha ushindani wenye tija kwenye bidhaa wanazozalisha," alisema.

Msasalaga alisema maandalizi, usimamizi na tathmini ya tuzo hizo yanafanywa na kamati maalum ambayo inahusisha taasisi mbalimbali ikiwamo Wizara ya Viwanda na Biashara, Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), TBS, ZBS, Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA), NQA na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE).

Alisema miongoni mwa vigezo vinavyotumika kuwapata washindi ni pamoja na nini kinafanywa na taasisi husika au mtu binafsi kuongeza ubora wa bidhaa, huduma, ufanisi katika uzalishaji au utendaji kazi kwa ujumla.

Mwakilishi kutoka TPSF, Gasper Kahungya alisema mashindano hayo ni muhimu kwan kuwa yataongeza chachu ya ushindani kwenye soko hasa kwa wazalishaji wa bidhaa walioko sekta binafsi.

Alipongeza TBS kwa kuandaa mashindano hayo ambayo ni muhimu kwa sekta binafsi na nchi kwa ujumla hasa katika kuhakikisha upatikanaji bidhaa bora zinazozalishwa nchini.

Mratibu wa Tuzo za Ubora TBS, Baraka Mbajije, alisema mchakato wa namna ya kushiriki mashindano hayo ni kujaza fomu ambazo zinapatikana katika tovuti ya TBS, TPSF pamoja na ZBS. Mhusika atajaza fomu na kutia saini kwa kuzingatia maelezo kulingana na kila kundi la ushiriki.

# Kanzidata ya utafiti kuanzishwa

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Watafiti Tanzania (ATARE) kinatarajia kuanzisha kanzidata ya kukusanya utafiti uliofanywa na wataalamu mbalimbali nchini na kuufanyia kazi ili usaidie kuleta suluhisho la changamoto.

Kanzidata hiyo pia itafanya kazi ya kukusanya wabobezi wote wa taaluma hiyo na kuwaweka pamoja ikiwamo kuwaunganisha na fursa mbalimbali za ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kupanua wigo na ubora wa utafiti unaofanywa nchini.

Jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Rais wa ATARE, Prof. Joseph Ndunguru alibainisha hayo wakati wa uzinduzi rasmi wa chama hicho.

Prof. Ndunguru alisema watafiti waliopo nchini wamekuwa wanafanya utafiti mara kwa mara, lakini asilimia kubwa ya kazi hizo za kitafiti hazijulikani ziliko.

Alisema hakuna nchi yoyote inayoweza kuendelea au kukua zaidi kiuchumi pasipo kuwa na utafiti bora wa kusaidia kwenye maeneo ya uzalishaji.

"Tunataka utafiti uliofanywa na unaoendelea kufanywa usaidie kutatua changamoto na matatizo yaliyoko kwenye sekta mbalimbali nchini na siyo kuhifadhiwa tu huko makabatini, hakuna nchi yoyote iliyoendelea pasipo mchango wa utafiti.

"Kwa mfano, baadhi ya mazao yanayolimwa nchini, inapofika wakati wa mavuno, yanavunwa nusu, ile nusu nyingine inabaki ardhini kwa sababu ya kukosa majibu ya dhana gani bora watumie ili wasipoteze mazao. Kwahiyo, katika hayo na mengine tunahitaji kuwa na utafiti bora za kusaidia," alisema Prof. Ndunguru.

Vilevile, Prof. Ndunguru alisema bado kuna uhitaji wa kuwekeza zaidi katika eneo hilo la utafiti nchini. Utafiti umekuwa unahitaji fedha nyingi na hivyo wengi kushindwa kufanikisha au kukamilisha kutokana na kukosa kipato.

"Na ndio maana tumeamua kuanzisha chama hiki, kwa sababu miongoni mwa mambo ambayo tutakuwa tunayajadili ni eneo hilo la namna ya kupata fedha kufanikisha utafiti wote muhimu kwa manufaa ya nchi yetu," alisema Prof. Ndunguru.

Aliwataka watafiti kujiunga na chama hicho na kwamba kama ilivyo katika taaluma nyingine, kitarahisisha kujadili changamoto zao na namna ya kuzitatua.

Mmoja wa watafiti wa chama hicho, Dk. Elizabeth Maeda, alisema chama hicho kitasaidia kuunganisha watafiti ambao watakuwa na nia njema katika kusaidia maendeleo ya nchi yao.

# NIT kuongeza utafiti wa ubia na taasisi kimataifa

**Na Prosper Makene**

MWENYEKITI wa Baraza la Uongozi la Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Prof. Ulingeta Mbamba amesema wataendelea kuingia katika makubaliano na taasisi mbalimbali za kimataifa ikiwa ni pamoja kuongeza fedha zaidi kwa ajili ya utafiti.

Prof. Mbamba ambaye hivi karibuni aliteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kushika nafasi ya uenyekiti wa Baraza la Uongozi wa NIT, alitoa shukrani zake kwa uteuzi huo na kusema kuwa anatarajia makubwa kwa kushirikiana na wajumbe wa baraza na wadau wengine ili kuendeleza malengo ya taasisi hiyo.

"Kwanza kabisa, ningependa kutoa shukrani zangu kwa uteuzi huu. Nimekubali jukumu nililokabidhiwa na kuahidi kufanya kila niwezalo. Ninatarajia kushirikiana na wajumbe wa baraza na wadau wengine ili kuendeleza malengo ya taasisi.

"Ninaahidi kufanyia kazi dhamira na dira ya taasisi kwa kuendeleza uwazi, uwajibikaji na uamuzi wenye ufanisi katika baraza," aliahidi.

Alisisitiza kuwa katika uongozi wake atahakikisha chuo kinaendelea kuwandaa vyema wanafunzi ili wafanye kazi sehemu yoyote duniani na kwa ufanisi wa hali ya juu.

"Nitajitahidi kuimarisha uhusiano kati ya NIT na waajiri. Hii ni pamoja na kuwapa wanafunzi wengi nafasi ya kufanya mafunzo katika kampuni na kusaidia kampuni kutafuta suluhu ya matatizo yao kupitia ushirikiano wa utafiti.

"Kama Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi, nina jukumu la kuongoza bodi na kuelekeza katika masuala ya kimkakati, kusimamia shughuli za kitaaluma na kiutawala za taasisi na kuhakikisha kunakuwa na utawala bora," alisema.

Aliongeza kuwa serikali imewekeza fedha nyingi katika miradi ya usafirishaji ikiwamo reli ya kisasa (SGR), Kampuni ya Ndege (ATCL) na ujenzi wa miundombinu kama viwanja vya ndege, barabara yakiwamo madaraja. Miradi hiyo yote inahitaji rasilimali watu ya kutosheleza usimamizi wake.

"Kwa dhati kabisa, nitashirikiana na baraza kuhakikisha kuwa chuo chetu kinaendelea kutoa elimu ya kiwango cha kimataifa kwa wanafunzi watu.



# Maudhui kupinga ukeketaji kwa watoto yaandaliwa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHIRIKA la Voice of Masai, limeandaa maudhui yaliyojikita kupinga vitendo vya ukeketaji kwa watoto wa kike, kuelimisha jamii ya kimasai kuwapeleka watoto wa shule na kuhamasisha ulinzi wa ardhi inayomilikiwa na jamii hiyo.

Maudhui hayo ni kwa ajili ya vijiji vilivyoko mikoa ya Kanda ya Kaskazini.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Ofisa kutoka Voice of Masai, Jeremy Evans, alisema shirika hilo linafanya kazi kwa kuifikia jamii ya kimasai ikiwamo kuibua vipaji mbalimbali walivyonavyo.

Aidha, alisema wamekuwa wakielimisha jamii hiyo kuhusu masuala yanayowahusu wamasai ikiwamo kuibua changamoto zinazowakabili.

Ofisa huyo, alisema lengo la kuanzishwa kwa Voice of Masai ni kuibadilisha jamii na mtazamo wao kupitia ujumbe mbalimbali sambamba na kuwanufaisha wahusika badala ya kufanya kazi ya pasipo kupata manufaa.

Pia, alisema kupitia kuibua vibaji hivyo, ikiwamo vya muziki wamefanikiwa kuwawezesha wasanii kurekodi nyimbo kwa lugha ya kimasai ambazo zimebeba ujumbe na maudhui ya jamii hiyo.

Pia, alisema mbali na uandaaji wa maudhui hayo kwa lugha ya kimasai pia wamekuwa wakitumia lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo, alisema hadi sasa shirika hilo limetimiza miaka 10 tangu kuanzishwa kwake ambapo walifika Tanzania kutembelea vivutio vya utalii ikiwamo Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngororongo(NCAA), walivutiwa na utamaduni wa kabila hilo.

Alisema baada ya kuvutiwa na utamaduni wa kabila hilo, waliridhia kuendeleza vipaji vya wamasai kama sehemu ya kutunza historia yao pamoja na kuwasaidia kujikwamua na matatizo mbalimbali yanayowakabili.

Alisema: "Miaka 10 iliyopita Voice of Masai walipokuja Tanzania kutembelea vivutio vyetu vya utalii walivutiwa na utamaduni wa kimasai na walituahidi kuendelea kuendeleza vipaji vyetu na kuisaidia jamii yetu kuondokana na matatizo yanayowakabili".



Ofisa Tarafa ya Kwekivu, Wilaya ya Kilindi, Mkoa wa Tanga, Michael John (kushoto) akiwaamuru vijana aliowakuta wakichimba dhahabu kinyume cha sheria ya madini katika Mto Mafueni ulioko kijiji cha Pagwi. Ofisa akiwa na wajumbe wa serikali ya kijiji hicho walivamia eneo hilo baada ya kulalamikiwa na wafugaji kuhusu uchafuzi wa maji yanayotumiwa na mifugo na matumizi ya binadamu. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Serikali yapiga 'stop' uchimbaji dhahabu Mto Mafueni

**Na Dege Masoli,** KILINDI

SERIKALI imesimamisha shughuli za ufyekaji na ukataji wa miti katika Msitu wa Lugirigiri pamoja na uchimbaji wa dhahabu kwenye Mto Mafueni, lengo kuu likiwa ni kudhibiti uharibifu mkubwa wa mazingira uliojitokeza hadi kufikia sasa.

Eneo lililoathirika zaidi na shughuli za binadamu ni vitongoji vyote vilivyoko Kata ya Pagwi wilayani hapa. Uamuzi wa kusitisha shughuli hizo ulitangazwa mwishoni mwa wiki na Ofisa Tarafa ya Kwekivu, Wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga, Michael John.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, serikali imeamua kuzuia shughuli hizo baada ya msitu huo kuvamiwa na zaidi ya ekari 20 kufyekwa na miti kuangushwa, huku serikali ya kijiji hicho ikiwa haina taarifa na shughuli zinazoendelea kwenye eneo hilo.

Akizungumza na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji cha Pagwi, baada ya kutembelea eneo la msitu huo na Mto Mafueni, Michael, alisema lengo la kusimamisha shughuli hizo ni kutaka kujiridhisha uhalali wa wahusika.

"Nyinyi ndiyo viongozi wa kijiji hiki, kama hamjui kinachoendelea serikali haiwezi kukaa kimya kuangalia uharibifu mkubwa kiasi kile unaofanywa na watu ambao hawajulikani wamepataje maeneo haya maana yanaonekana ni msitu na siyo shamba la mtu," alisisitiza.

Kuhusu uchimbaji dhahabu kwenye Mto Mafueni, Ofisa huyo alisema ni kosa kisheria kuchimba dhahabu bila ya kuwa na kibali cha Kamishna wa Madini wa eneo husika.

Kutokana na kukosekana kwa uhalali huo, amewataka wahusika kufuata kanuni, taratibu zilizopo ili serikali nayo iweze kupata haki yake.

Alipoulizwa kuhusu uharibifu huo wa mazingira, Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji hicho, Mussa Masali, alikiri kwamba tatizo hilo linatokana na watu kutofuata sheria na kwamba maeneo hayo yalishapigwa marufuku na serikali ya kijiji, lakini bado wananchi wanakaidi amri hiyo.

Masali alieleza kuwa kwa sasa Serikali ya Kijiji haitasita kuchukua hatua kali kwa mtu yeyote atakaekwenda kinyume na maelekezo yanayotolewa na viongozi, lengo ni kulinda vyanzo vya maji na hifadhi ya misitu.

Kiongozi wa jamii ya wafugaji wa Kimasai katika eneo hilo, Alaigwanani, Soda Kimilei, alimshukuru ofisa pamoja na Serikali ya Kijiji kwa hatua iliyochukuliwa, kwamba uchafuzi wa mazingira katika mto huo ulikuwa kero kubwa kwa wafugaji kutokana na mifugo kunywa maji machafu yanayotokana na uchimbaji huo wa dhahabu.

## Waomba barabara kuwekwa matuta kuwanusuru kugongwa

**Na Steven William,** MUHEZA

KATIKA kipindi cha miaka 22, watu 16 katika Kijiji cha Mpakani, Kata ya Kwakifua wilayani Muheza mkoani Tanga wamefariki dunia kwa kugongwa na magari.

Idadi hiyo wamo watoto na wanafunzi wanaovuka kwenda shule nyakati za asubuhi na jioni katika Barabara ya Tanga Mjini kuelekea Segera.

Kutokana na hali hiyo, wakazi hao wameiomba serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Tanga kujenga matuta katika sehemu hiyo.

Walifikisha kilio chao kwa Mkuu wa Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani wilayani Muheza, Reonard Bandora ambaye alifika kijijini hapo kutoa elimu ya usalama barabarani.

Katibu wa Umoja wa Vijana CCM, kijijini hapo, Mbarouku Mohamed alisema kwa kipindi cha mwaka 2001 mpaka 2023 katika kijiji hicho watu 16 wamefariki dunia kwa kugongwa na magari.

Alisema kutokana na matukio hayo wameiomba serikali kuwajengea matuta, kuchora alama za barabarani za wavuka kwa miguu yani pamoja na kuwekewa kibao cha kidhibiti mwendo katika eneo hilo.

Alisema pia wanaomba kuwepo na askari wa usalama barabarani.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Mayasa Kilua, alisema mwaka huu tayari watu watano wamefariki dunia kwa kugongwa na magari.

Naye Kamanda Bandora alisema wamesikia kero hiyo na kuwaahidi wananchi hao kwamba ataandika barua kupeleka TANROADS Mkoa wa Tanga kuangalia uwezekano wa kuweka matuta.

Alisema kuwa pia atawataarifu kufika katika eneo hilo na kuweka alama za barabarani.

Kadhalika, aliwaasa wananchi hao kuwa na uangalifu wa matumizi ya barabara pindi wanapovuka.

## NCAA yaridhia ombi la kuongezwa malango mapya ya utalii

**Na Godfrey Mushi,** NGORONGORO

MENEJIMENTI ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), imeridhia ombi la muda mrefu la wadau wa sekta ya utalii nchini, la kutaka kuongezwa kwa malango mapya ya utalii katika eneo la Engaruka na Eyasi.

Kwa mujibu wa Naibu Kamishna wa NCAA, anayeshughulikia uhifadhi, utalii na maendeleo ya jamii, Elibariki Bajuta, uamuzi huo pamoja na mambo mengine, unalenga uboreshaji wa huduma kwa watalii wanaoingia ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Alidokeza kuhusu mpango wao wa kufungua malango mapya, wakati wowote kuanzia sasa, alipokutana na viongozi Chama cha Waongoza Utalii Tanzania (TTGA), waliotembelea NCAA mwishoni mwa wiki.


Bajuta, alisema lengo la serikali ni kuboresha huduma kwa wageni wanaoingia ndani ya hifadhi, kuongeza mtawanyiko kwenye vivutio vya utalii na kupunguza msongamano wa wageni katika lango la Loduare na barabara kuu ya Loduare, Seneto hadi Golini, ambapo ni mpakani mwa NCAA na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Alisema maeneo yatakayofunguliwa malango hayo ni Eyasi, ambapo ujenzi wa lango umekamilika na kazi zinazoendelea ni kusimika mifumo ya malipo, mtandao wa intaneti na uboreshaji wa barabara ya kutoka Eyasi kupitia Mlima Enduleni.

Kazi nyingine ni kuboresha pia miundombinu ya Barabara ya Ndutu hadi uelekeo wa Serengeti, ili wageni wanaokuwa eneo la Ziwa Eyasi kwa shughuli za utalii wa kiutamaduni wasilazimike kurudi Karatu na kuingilia lango la Loduare kwenda Ngorongoro.

Alisema, lango la pili litajengwa mpakani mwa eneo la Engaruka na Empakaai-Kreta. Ujenzi huo unakwenda sambamba na kufungua barabara itakayoanzia Engaruka kuelekea Kreta za Empakaai, Olmoti Kreta, Mlima Lolmalasin hadi Kreta ya Ngorongoro.

Ujenzi wa malango hayo umenza mwaka huu wa fedha na utakamilika katika mwaka ujao wa fedha.






Naibu Waziri Mkuu, Dotto Biteko, akipata maelezo ya magari kutoka kwa Ofisa Masoko na Mawasiliano wa Kampuni ya Gf Trucks & Equipments Ltd, Smart Deus, alipokagua mabanda ya maonyesho ya madini mkoani Geita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jela miaka mitano kwa wizi wa kinanda cha kanisa

**Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Sengerema imemhukumu kwenda jela miaka mitano mkazi wa Mwabaruhi, Mussa Juma baada ya kumkuta na hatia ya kuiba kinanda mali ya Kanisa la Katoliki la Bitoto wilayani hapa.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu wa Mahakama hiyo, Tumsifu Barnabas, baada ya kumkuta na hatia mshtakiwa huyo na kosa moja kati ya matano yaliyokuwa yakimkabili.

Awali akieleza mashtaka ya mtuhumiwa huyo, Mwendesha mashtaka wa Jeshi la Polisi, Theophilus Bei, alieleza kuwa Mussa anakabiliwa na makosa matano.

Alitaja kosa la kwanza na la tatu ambalo alitenda Oktoba 25 mwaka jana ni kuvunja kanisa na kuiba kinanda, power mixture, spika moja, extension, genereta, adapter ana kitambaa mita nne, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 3.31.

Kosa la pili alitenda majira ya saa mbili na nusu asubuhi, alivunja na kuingia katika Kanisa la Wadventista Wasabato, kisha kuiba spika moja, power mixtute, kipaza sauti, diski moja, king'amuzi, extension mbili, pini soketi na kitambaa mita tano, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 2.34.

Akitoa hukumu ya kesi hiyo, Hakimu Tumsifu alielezea kuwa kati ya makosa hayo kosa la tano ndilo lililomtia hatiani kwa kukutwa na mali ya wizi nyumbani kwake.

Alisema mtuhumiwa huyo alikutwa na kinanda na kitambaa mita nne kilichokuwa kikitumika kufunikia kwenye kinanda kinyume na kifungu cha 311 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura Namba 20 toleo la 2022.

Alieleza kuwa mahakama hiyo imejiridhisha bila kuacha shaka kufuatia ushahidi uliofikishwa mahakamani hapo na kumhukumu kutumikia kifungo cha miaka mitano jela.

Pia Hakimu Tumsifu aliagiza kinanda na kitambaa vikabidhiwe kwa mmiliki ambaye ni Kanisa Katoliki la Bitoto.

## TRA yabaini mbinu mpya ya w'biashara kukweka kodi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) mkoa wa kikodi Kahama, imebaini mbinu mpya wanazozitumia baadhi ya wafanyabiashara katika ukwepa kodi, mojawapo ni kutumia Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) za pikipiki kusajili mashine za kielektroniki.

Inaelezwa kuwa TIN hizo zilizosajiliwa maalumu kwa ajili ya pikipiki ambazo hazilipiwi ushuru, zimekuwa zikitumika tena katika usajili wa mashine za kielektroniki na kutoa risiti bila kulipia kodi stahiki.

Kaimu Meneja wa TRA mkoa wa kikodi Kahama, Wisaka Kamwamu, alibainisha hayo hivi karibuni wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Tuwajibike yenye kauli mbiu 'Risti yako, Maendeleo yako" iliyofanyika katika Manispaa ya Kahama.

Alisema wengine wanadaiwa pia kununua risiti za kielektroniki mitaani na kuziambatanisha katika maombi ya fedha za VAT na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

"Alisema kwa wale ambao wamekuwa na tabia ya kutumia TIN za pikipiki katika utaoaji wa risti watawajibishwa kisheria ikiwemo kufunguliwa kesi za uhujumu uchumi na kuwataka na wale wanaofanya mchezo huo kuacha mara moja."

Kamwamu alisema lengo la kuwa na kampeni hiyo ni kuwakumbusha wafanyabiashara kudai na kutoa risiti za kielektroniki wakati wa biashara zao, kwamba wanapotumia vizuri mashine hizo zinawasaidia katika ukadiliaji wa kodi na kupata kiwango sahihi ambacho wanatakiwa kulipa, kuondoa malalamiko baina yao na TRA.

Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara na Viwanda na Kilimo (TCCIA), Charles Machari alipongeza serikali kwa kutengeneza mazingira mazuri dhidi yao akisema kila kukicha kumekuwa na wimbi kubwa la wafanyabiashara wadogo ambao wanatakiwa kuendelea kupewa elimu ya biashara na kutambua majukumu ya TRA.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita aliwataka wafanyabiashara wanaofanya vitendo vya udanganyifu katika biashara zao waache kabla msako haujaanza na kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Aidha, aliwataka TRA katika kampeni hiyo waanze kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mashine hizo kwa sababu kila siku kunaibuka wafanyabiashara wapya.

# Naibu Waziri ajinasibu kutatua kero za wawekezaji madini

**Na Jenesta Jasson,** NGARA

NAIBU Waziri wa Madini, Steven Kiruswa ameahidi kutoa ushirikiano katika utatuzi wa kero zinazowakabili wawekezaji katika sekta ya madini nchini, ikiwa ni pamoja na ubovu wa miundombinu, nishati na upatinaji wa maji katika miradi yao.

Alitoa ahadi hiyo juzi alipofanya ukaguzi wa mradi mpya wa tembo nickel uliopo katika Wilaya ya Ngara mkoani Kagera unaotarajia kuzalisha tani 58.

Alisema kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha wawekezaji wanafanya kazi katika mazingira rafiki na kuongeza pato la taifa.

Naibu Waziri Kiruswa alisema kuwa miongoni mwa changamoto alizozibaini katika maeneo ya uwekezaji ni pamoja na ukosefu wa umeme, miundombinu rafiki hivyo kuahidi kushirikiana na sekta husika katika kutatua kero hizo.

Aidha, alipongeza uongozi wa Kampuni ya Tembo Nickel kwa juhudi za upanuzi wa miradi ya madini na kuwaagiza kuhakikisha wanakamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi wote walioguswa na mradi huo, malipo ya fidia yaende sambamba na kuwaamisha walengwa.

Vilevile aliwataka wawekezaji hao kuhakikisha wanatoa fursa za ajira kwa wazawa wa eneo hilo na kueleza kuwa Rais Samia Suluhu Hassan anatarajia kuona mradi huo ukitekelezwa kwa kasi na kwa ubora wa hali ya juu.

Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Benedicto Busunzu, alisema kuwa mradi huo unatarajiwa kuzalisha tani milioni 58 za madini baada ya kuanza utekelezaji wake ambako ukomo wake utakuwa baada ya miaka 30.

Alisema kuwa mgodi huo utachukua eneo kubwa, kwamba utapitia kwa baadhi ya maeneo ya wakazi wa maeneo hayo ambao idadi yao ni 1,000 yakiwamo makazi 349 ambao watalipwa fidia zao hivi karibuni ili kupisha eneo hilo kwa ajili ya kuruhusu mgodi huo kuanza kazi.

Alitumia fursa hiyo kuiomba serikali kutatua changamoto zilizopo katika maeneo hayo ikiwamo ukosefu wa miundombinu mizuri kama vile barabara kuwa mbovu na ukosefu wa umeme kwenye eneo hilo. Mbunge wa Ngara, Ndaisaba George, aliishukuru kampuni hiyo ya Tembo Nickel kwa kuanzisha mradi katika eneo hilo na kuiomba kuwapa fursa wazawa wa eneo hilo ya kufanya kazi katika mradi huo na kutoa fursa kwa wafanyabiashara kutoa huduma mbalimbali ili kuongeza mzunguko wa fedha ndani na nje ya jimbo hilo.

Nipashe Spotika



SABABU 3 LIVERPOOL WANATAKIWA KUMUUZA MO SALAH JANUARI 2024 UK. 12-13



# WAINGEREZA WA5 BORA ZAIDI DUNIANI KWA SASA

RICE

**LONDON,** England

ENGLAND ina historia nzuri katika kiwango cha kimataifa na soka linaendelea kuwa chanzo cha furaha na fahari kwa taifa hilo. England ni nyumbani kwa Ligi Kuu maarufu kama EPL, shindano maarufu zaidi la klabu za hali ya juu duniani.

'Simba Watatu' ni jina la utani la kikosi cha Timu ya Taifa ya England kilichojaa wachezaji wenye vipaji vya hali ya juu. Kwa hakika, England wana kundi la vipaji vingi sana hivi kwamba kuna kadhaa wa hadhi ya juu ambao hukosa kila mara kuitwa kikosi cha taifa wakati wa mapumziko ya kimataifa au mashindano makubwa.

Kutoka kwa magwiji kama Sir Bobby Charlton na Gary Lineker hadi nyota wa kisasa kama Harry Kane na Wayne Rooney, wanasoka wa England wameonesha vipaji vyao katika mashindano ya kifahari.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano bora zaidi wa England duniani kwa sasa...

#### #5 Marcus Rashford (Manchester United)

Akiwa zao la Akademi ya Manchester United, Marcus Rashford, ni mmoja wa washambuliaji bora zaidi duniani kwa sasa. Mshambuliaji huyo anayesisimua anaweza kucheza popote kwenye mstari wa mbele na uwezo wake wa kuwashinda mabeki pamoja na ujuzi wake wa kufunga.

Rashford alifunga mabao 30 na kutoa asisti 11 katika mechi 56 alizocheza katika mashindano yote akiwa na Manchester United msimu uliopita. Pia alitoa mchango muhimu kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022, akifunga mabao matatu kwa 'Simba Watatu' kwenye mashindano hayo.

Kwa sababu ya wingi wa wachezaji wa safu ya ushambuliaji kwa Kocha Gareth Southgate, Rashford huwa haanzi mara kwa mara kwenye kikosi cha kwanza cha England. Hata hivyo, huwa anafanya kazi nzuri kila wakati anapopewa nafasi.

#### #4 Declan Rice (Arsenal)

Declan Rice ni mmoja wa viungo bora zaidi wa Ligi Kuu England. Arsenal walimnunua majira ya joto kwa kitita cha euro milioni 116.6 na ameanza vema maisha yake pale Emirates.

Rice ni kiungo mkabaji na mwenye akili. Amefaulu kusoma mtiririko wa mchezo na kuvunja mchezo. Mchezaji huyo wa zamani wa West Ham United pia ni mpiga pasi nadhifu na ni mzuri sana katika kuendeleza mpira pia.

Amekuwa mchezaji kwenye kikosi cha kwanza cha England katika miaka ya hivi karibuni na mtindo wake wa uchezaji mzuri na umekuwa na jukumu muhimu katika hilo.

#### #3 Bukayo Saka (Arsenal)

Katika kipindi cha msimu wa 2022-23, Bukayo Saka alijiimarisha kama mmoja wa mawinga bora zaidi duniani. Mwingereza huyo ana ubora, wepesi na ustadi wa kuteleza.

Saka huharibu winga ya kulia kwa klabu na nchi na kwa kawaida huwa mwiba kwenye shingo ya mabeki. Ana uwezo wa kukata ndani kutoka pembeni na kuweka mpira nyuma ya wavu kama vile anaendesha gari hadi mstari wa mbele kabla ya kutoa krosi murua.

Saka alifunga mabao 15 na kutoa pasi za mabao 11 katika mechi 48 alizocheza kwenye michuano yote akiwa na Arsenal msimu wa 2022-23.

#### #2 Harry Kane (Bayern Munich)

Harry Kane ni mmoja wa washambuliaji bora wa kizazi chake. Mshambuliaji huyo wa kati wa England hatimaye alifanikiwa kuhamia Bayern Munich mapema msimu huu wa majira ya joto na anaweza kushinda taji kubwa kwa mara ya kwanza katika maisha yake ya soka. Kane amekuwa mmoja wa wafungaji mabao wengi zaidi kwenye sayari hii katika kipindi cha miaka 10 iliyopita.

Alikuwa katika kiwango kizuri kwa klabu yake msimu uliopita licha ya Tottenham Hotspur kuvumilia kampeni ngumu. Kane alifunga mabao 30 na kutoa asisti tatu katika mechi 38 za Ligi Kuu msimu uliopita.

Ameanza vema maisha katika Klabu ya Bayern Munich na anatarajiwa kuwa na jukumu muhimu kwa 'Bavarian' hao kwani wanataka kushinda mataji mengi msimu huu. Tayari amefunga mabao saba katika mechi zake tano za kwanza Bundesliga.

#### #1 Jude Bellingham (Real Madrid)

Jude Bellingham ana umri wa miaka 20, tu lakini tayari ni mmoja wa viungo bora zaidi duniani. Real Madrid walipata huduma yake kwa kitita cha euro milioni 103 msimu huu wa majira ya joto na inaonekana wamefanikiwa kutokana na uchezaji wake katika wiki za mwanzo za kampeni mpya.

Bellingham amekuwa moto wa kuotea mbali kwa Real Madrid katika msimu mpya, akifunga mabao matano na kutoa asisti katika mechi nne hadi sasa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ni mtu asiyechoka uwanjani na pamoja na sifa zake za kiufundi, pia anaonesha uelewa wa kimbinu na ustadi wa uongozi ambao unadharau umri wake.

### ISIKUPITE

HAT-TRICK (mabao matatu), aliyofunga Harry Kane wakati Bayern Munich ikiichapa VfL Bochum 1848 mabao 7-0 kwenye Bundesliga Jumamosi ilikuwa hat-trick yake ya kwanza kwenye ligi ya tangu Desemba 2017, alipofunga mfululizo kwa Tottenham dhidi ya Burnley na Southampton, lakini pia yanamfanya kufikisha mabao saba katika mechi zake tano za kwanza za Bundesliga.



## Extra Time

# SABABU 3 LIVER WANATAKIWA KUMUUZA SALAH JANUARI 2024



**LIVERPOOL,** England

KWA Liverpool, kufungwa kwa dirisha la uhamisho la Saudi Arabia kulikuwa na ahuweni. Baada ya mipango yao ya kujenga upya safu ya kiungo, hawakuweza kuwa tayari kumpoteza Mohamed Salah mwishoni mwa dirisha la usajili.

**Baada ya kuondoka kusikotarajiwa kwa Fabinho na Jordan Henderson, tayari walikuwa wanahaha kutafuta kuimarisha nafasi ya kiungo. Kumpoteza Salah kungekuwa kifo cha matarajio yao msimu huu.**

Licha ya matarajio madogo ya kujiandaa na msimu mpya, Klopp bado anaamini kuwa kikosi chake kina uwezo wa kuwapa changamoto Manchester City kuwania taji la Ligi Kuu England. Na kwa hilo, atamhitaji Salah sasa kuliko wakati mwingine wowote.

Lakini, vipi ikiwa Liverpool watampoteza Salah katika dirisha la usajili la Januari 2024? Na ikiwa hivyo, je, utakuwa mwisho wa kutamba kwa Wekundu hao? Makala haya yanaangalia sababu tatu kwa nini Liverpool inaweza kufaidika na mauzo ya Salah Januari 2024.

### #1 Thamani ya uhamisho ya pauni milioni 200

Klabu zinazosimamiwa na Mfuko wa Uwekezaji wa Umma wa Saudi Arabia si za kushindwa kumsajili mchezaji wanayemtaka kweli. Kwao, mfuko wa dola trilioni unahakikisha ugavi wa kutosha wa fedha. Kwa hiyo, ni suala la muda tu kabla ya kuwavutia walengwa wao kwa malipo makubwa.

Iwapo waliweza kutumia zaidi ya pauni milioni 200 kumnunua Ronaldo, ambaye ni zaidi ya kiwango chake cha ubora kwa sasa, bila shaka wanaweza kutumia zaidi ya pauni milioni 200 kumnunua Salah, ambaye bado ni mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani. Ofa kama hiyo kwa mchezaji mwenye umri wa miaka 31, ambaye amebakiza miaka miwili pekee kwenye mkataba wake itakuwa ngumu sana kwa kwa Liverpool kuikataa.

Ingawa Liverpool hawajatumia fedha nyingi kama Chelsea na PSG, wamefanya vema kutengeneza kikosi ambacho kinaweza kumwangamiza mpinzani yeyote.

Liverpool wanaweza kupata pauni milioni 250 katika ada ya uhamisho na mishahara kutokana na kuondoka kwa Salah.

Liverpool wanaweza kuunda kikosi cha siku zijazo kwa fedha nyingi bila kuwa na wasiwasi juu ya ada ya uhamisho kwa walengwa wengine.

Januari 2018, Liverpool walimruhusu Philippe Coutinho kujiunga na Barcelona baada ya ofa ya uhamisho ya pauni milioni 14 kutoka Barcelona.

Fedha hizo ziliweka msingi wa mafanikio ya Liverpool kwa miaka mingi kwani Virgil Van Dijk na Alisson Becker waliwasaidia kushinda kila taji kuu ambalo Liverpool ilishindania.

Jambo kama hilo linaweza kutokea ikiwa 'Wekundu' hao watafikiria kumuuza Salah kwa kiwango kinachofaa cha fedha. Wamefanya kazi kwa ustadi kwenye dirisha la uhamisho katika siku za hivi karibuni. Kwa hiyo, hakuna sababu kwa nini hawataweza kulenga wachezaji bora wakati huu pia.

### #2 Hali ya mkataba wa Salah

Kwa klabu kuruhusu wachezaji kuendelea hadi mwaka wa mwisho wa mkataba wao sio hali nzuri. Ikiwa mchezaji anataka kuhama, basi klabu haina chaguo ila kuwauza kwa bei ya chini.

Wachezaji, wakati huo huo, wanaweza kufaidika sana na hali kama hiyo kwani wanaweza kumaliza mikataba yao au kuhamia klabu wanayoipenda kwa bei nzuri. Kwa njia hiyo, wanaweza kupata mishahara mikubwa kutoka kwa waajiri wao wapya.

Hivi sasa, Salah ana mkataba wa miaka miwili pale Anfield. Lakini, haya yote yanaweza kubadilika mara tu atakapoingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake msimu ujao wa majira ya joto. Ingawa hajaonesha nia ya kuondoka Anfield hadi sasa, lolote linaweza kutokea ndani ya mwaka mmoja.

Iwapo Liverpool wanataka kuepuka hali hii, wanaweza kumuuza Salah ikiwa ofa sahihi itafika Januari. Wana muda wa kutosha kati ya sasa na kisha kutafuta mbadala. Inaweza kuwa hali ya ushindi wa pande zote mbili

### #3 Wakati wa kutafuta mrithi wake

Pamoja na kipaji chake na kujitolea kwake katika klabu, Salah atafikisha umri wa miaka 32, msimu ujao utakapoanza. Huku Wekundu hao wakizingatia zaidi kizazi cha vijana kuongoza klabu hiyo.

Hapo awali, Liverpool walihama haraka kutoka kwa wachezaji ambao walikuwa wakizeeka au hawakuwa na nia ya kutumia kiasi kikubwa cha maisha yao ya baadaye hapo Merseyside. Wachezaji kama Sadio Mane, Roberto Firmino, na Gini Wijnaldum waliachiwa.

Ingawa Salah, labda, amekuwa mchezaji bora zaidi kwa Liverpool kuwahi kuwa naye, kumshikilia hakutakuwa na maana sana kwa muda mrefu. Washambuliaji huwa wanapungua haraka kwa sababu baada ya muda, wanapoteza kasi na wepesi.

Ingawa Salah bado hajapoteza uwezo wake mwingi na amebaki bila majeraha kwa muda mrefu, itakuwa ngumu kwake kuendelea na kasi hii. Liverpool tayari wamejenga upya safu yao ya ushambuliaji kwa kuwanunua Diogo Jota, Darwin Nunez, na Luis Diaz. Kumwacha Salah aondoke kunaweza kuwa baraka.

Kuondoka kwa Salah Januari kunategemea mambo mbalimbali.

Kwa Salah Januari inategemea sana nafasi ya Liverpool kwenye msimamo wa Ligi Kuu England. Ikiwa timu ya Klopp itasalia kwenye mkondo wa kunyakua taji la Ligi Kuu, hakuna njia ambayo Salah atauzwa Januari.

Lakini Liverpool haitakuwa kwenye nafasi sahihi kati ya sasa na Januari, basi klabu inaweza kujaribiwa kumuuza.

Mbali na hilo, jinsi Liverpool wana muda wa kutosha kati ya sasa na Januari kutafuta mbadala wake. Kwa hiyo, ikiwa watapanga vizuri, wanaweza kuchukua nafasi yake mnamo Januari wakati pia wakiwa na fedha za kutosha kwa siku zijazo.

Lakini endapo mchezaji huyo mpya atafikia kiwango cha chini, Liverpool watapata matokeo mabaya uwanjani. Pia wanaweza kushindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

## Nukuu

"Ninapenda jinsi alivyo. Ninapenda jinsi anavyotaka zaidi kutoka kwake mwenyewe, hafurahii tu jinsi alivyo, na bado ni mchanga sana na ni wazimu kusema hili. Na alichofanya mwaka jana, sidhani kama tutaona tena kuwa waaminifu isipokuwa avunje rekodi yake mwenyewe. Anauhitaji sana, na ikiwa tunaweza kumpata katika maeneo hayo, tunajua daima atakuwa katika nafasi sahihi. Ana silika hii ya kufunga bao, ni raha tu kucheza na mtu ambaye ni mzuri hivi," **Kiungo wa Manchester City, Phil Foden akidai rekodi ya mabao ya 36 katika mechi 35 msimu uliopita ya Erling Haaland, haitavunjwa.**




"Hapana, nitasema kwa nini. Ninakukumbusha nilipofika mwanzoni (kama mchambuzi) huko Amazon, nilisema "Kwangu kucheza katika timu hii, ni maumivu ya kichwa. Nilizungumza juu ya muundo. Unachezaje na wote watatu (Messi, Neymar, na Mbappe) kwa wakati mmoja?Alipocheza (Messi) na timu ya Argentina, (kulikuwa na) muundo. Hakuna Messi watatu, yeye tu. Unamweka katika mfumo ambapo yeye peke yake ndiye bosi (na atang'ara)," **Nyota wa zamani wa Arsenal na Ufaransa, Thierry Henry, akieleza namna ilivyokuwa ngumu kwa PSG kuwachezesha Lionel Messi, Neymar, na Kylian Mbappe ndani ya kikosi kwa wakati mmoja.**



"Natumai Rodri atajifunza. Anapaswa kudhibiti hisia zake. Sipendi kucheza dhidi ya 10. Leo yeye si kiungo bora zaidi duniani," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, akishindwa kuficha masikitiko yake baada ya kiungo waka Rodri kutolewa nje kwa kadi nyekundu katika ushindi wao wa mabao 2-0 wa Ligi Kuu England dhidi ya Nottingham Forest Jumamosi.**






AZIZ KI

# MABAO MATANO MAKALI YA FAULO LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara iko kwenye raundi ya tatu kwa mechi 24 kupigwa jumla ya mabao 57 yamefungwa mpaka sasa.

**Mabao 13 kati ya hayo yamefungwa nje ya boksi, manane yakiwa ni ya wachezaji kukokota mpira na kupiga mashuti na matano ni ya faulo.**

Katika makala haya tutayaangalia mabao matano ya faulo yaliyofungwa kwenye Ligi Kuu mpaka sasa na wachezaji mbalimbali. Wachezaji watano waliofunga mabao kwa mipira ya kutengwa wawili ni wa kigeni na watatu ni wazawa.

**1. Martin Kigi (JKT Tanzania vs Namungo)**

Anashikilia rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga kwa mkwaju wa faulo msimu huu wa 2023/24. Kigi, mchezaji wa Kitanzania alifanya hivyo kwenye mechi ya ufunguzi Agosti 15, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi, timu yake ya JKT Tanzania ikicheza dhidi ya wenyeji, Namungo FC.

Aliipa timu yake bao la ushindi na la pekee kwenye mchezo huo kwa mkwaju wa faulo kiasi cha mita 25 hivi kutoka langoni mwa wapinzani wao.

Ilikuwa ni faulo ya dakika ya 43, iliyopigwa pembeni winga ya kushoto na hakupiga shuti kali, ila alitumia akili ya kuupiga kwa kukata na mpira kwa mguu wa kulia, ukamzubaisha kipa Jonathan Nahimana licha ya kutaka kuudhibiti mikononi, ulimponyoka na kujaa wavuni.

**2. Ibrahim Ajibu (Coastal vs Mtibwa)**

Kiungo wa zamani wa timu za Simba na Yanga, Ibrahim Ajibu anaingia kwenye rekodi ya kuwa mmoja wa wachezaji waliofunga mabao kwa faulo msimu huu, akifanya hivyo Agosti 20, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani Morogoro, timu yake ikicheza dhidi ya Mtibwa Sugar.

Madhambi yalitokea karibu na mstari wa pembeni winga ya kulia na pia ilikuwa mbele kidogo ya duara la kuanza mpira, kiasi mita zipatazo 40 hivi na kuwa moja ya mabao ya faulo yaliyofungwa mbali zaidi.

Ajibu, mchezaji wa Kibongo, alitumia mguu wake wa kulia dakika ya 69 kupiga mpira juu kuelekea Kaskazini mwa uwanja baada ya kugundua kuwa kipa Mohamed Makaka alikuwa mbele sana ya lango.

Hesabu zake zilikuwa sahihi mpira ukajaa ndani ya lango. Kassim Haruna alisawazisha bao dakika ya 83 mechi ikaisha 1-1.

**3. Stephane Aziz Ki (Yanga vs JKT Tanzania)**

Kama ilivyofanya kwa Namungo, JKT Tanzania ililizwa na Yanga ilipofungwa bao la mkwaju wa faulo la Stephane Aziz Ki, Agosti 29, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Ilikuwa imebaki sekunde chake kabla ya mechi kuwa mapumziko. Yeye mwenyewe ndiye aliyeangushwa nje kidogo ya eneo la hatari karibu na nusu mduara wa lango la Kusini mwa uwanja.

Aliachia shuti kwa mguu wa kushoto ambalo alilinyanyua juu ya vichwa vya wachezaji wa JKT Tanzania na wa Yanga, mpira ukaenda moja kwa moja wavuni. Yanga ikishinda mabao 5-0 katika mechi hiyo.

**4. Omari Kindamba (Mashujaa vs Ihefu)**

Faulo aliyopiga Kindamba, mchezaji wa Kitanzania haitofautiani na ile ya Ajibu. Na hizi mbili licha ya ufanano wake ndizo faulo zilizopigwa kutoka mbali zaidi.

Ilipigwa kiasi cha mita 40 hivi pembeni kabisa mwa uwanja karibu na chaki, upande wa kulia kuelekea lango la Kusini la Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma.

Akitumia mguu wa kulia aliunyanyua mpira juu kuelekea kwenye lango la Ihefu. Wakati huo kipa Fikiri Bakari alikuwa hapo hapo langoni ni kama hakuuona kutokana na kupigwa na jua usoni kwani alipoushtukia upo karibu, alipeleka mikono yake juu, lakini alichelewa, mpira ulikuwa umeshapita. Mashujaa ilishinda mabao 2-0.


**5. Cheikh Sidibe (Azam vs Singida)**

Mechi ilichezwa Alhamisi iliyopita Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam. Azam ilipata faulo dakika ya tisa ya mchezo na ilikwenda kupigwa na kiungo raia wa Mali, Sidibe.

Ilifanyika mita zipatazo 30 hivi kuelekea kwenye lango la Singida Fountain Gate alichia shuti kali kwa mguu wake wa kushoto, kipa Beno Kakolanya alijinyoosha na kuruka juu kufuata mpira, lakini ni vidole vyake tu ndivyo vilivyofanikiwa kugusana na mpira uliompita na kujaa wavuni.

Lilikuwa ni bao la pili kwa faulo kufungwa kwa mguu wa kushoto baada ya Aziz Ki. Hii ina maana wachezaji wote wawili wa kigeni wamefunga kwa kutumia mguu wa kushoto na Watanzania kulia. Azam ilitoka na ushindi wa mabao 2-1.

**JE, WAJUA?**



KIUNGO mpya wa Real Madrid, Muingereza Jude Bellingham, tayari ameifungia timu yake hiyo mabao matano katika mechi nne na kutoa asisti tangu ajiunge na timu hiyo majira haya ya joto.





# Matukio ya rushwa yamchefua kiongozi Mwenge wa Uhuru

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IRAMBA

KIONGOZI wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2023, Abdalla Shaibu Kaim amesema kuwa miradi mingi ya maendeleo inakwama kutokana na watekelezaji au wasimamizi kuendekeza vitendo vya rushwa.

Kutokana na hali hiyo, amewataka Watanzania kukemea vitendo vya rushwa akisema vinakwamisha maendeleo ya maeneo yao na Taifa kwa ujumla.

Aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kata ya Kiomboi Wilaya ya Iramba mkoani Singida muda mfupi baada ya kumaliza kukagua, kuzindua na kuweka jiwe la msingi kwenye miradi ya maendeleo inayotekelezwa wilayani humo.

Kaim alisema ili kuwa na miradi bora na yenye kukubalika ni lazima kila mtanzania kupinga vitendo viovu vya utoaji au upokeaji wa rushwa na kusababisha miradi au huduma kuwa chini ya ubora.

Alisema tatizo la rushwa bado lipo nchini na imefika wakati Watanzania wanaweza kuichukia serikali yao kwa kukosa huduma nzuri pale mmoja anapokuwa amepokea rushwa au kutoa rushwa kwa kuwa rushwa inapotosha haki.

Kuhusu utunzaji wa mazingira, aliwataka Watanzania kutunza mazingira ili kuepuka kupata magonjwa yanayosababishwa na uchafu na kuepukana na kufanya shughuli za kibinadamu katika maeneo yenye vyanzo vya maji.

Alisema kwa sasa kuna mabadiliko ya tabia nchi, hivyo ni vyema Watanzania wote kwa ushirikiano wanatunza vyanzo vya maji na kukaa zaidi ya mita 60 zaidi ya chanzo cha maji.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba akipokea Mwenge wa Uhuru kutokea mkoani Tabora, alisema unatarajiwa kutembelea kuzindua pamoja na uwekaji wa mawe ya msingi miradi yenye thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 224 ambayo imetekelezwa katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Septemba 2023.




Naibu Waziri Mkuu, Dotto Biteko (wa pili kulia), akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Benki ya Azania tawi la Geita, Rhoda Baluhya (kushoto), alipotembelea banda la benki hiyo kwenye Maonesho ya Sita ya Kimataifa ya Teknolojia ya Madini yanayoendelea jijini Geita. Maonesho hayo yamefunguliwa rasmi na Naibu Waziri Mkuu mwishoni mwa wiki. Wengine pichani ni Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (kulia), Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martin Shigela (wa tatu kulia).
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Paroko ahimiza umoja kudhibiti mmomonyoko wa maadili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KUTOKANA na ongezeko la vitendo vya mmomonyoko wa maadili nchini ikiwamo ndoa za jinsia moja, Watanzania wametakiwa kuwa mstari wa mbele kupinga hali hiyo badala ya kuwaachia viongozi wa serikali pekee yao.

Paroko wa Parokia ya Kiwanja cha Ndege Jimbo Katoliki la Dodoma, Emmanuel Mutambo, alitoa kauli hiyo jana jiji hapa kwenye Tamasha la Uinjilishaji lililoandaliwa na Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA) wa Parokia hiyo.

Alisema hivi sasa vitendo vya mmomonyoko wa maadili nchini vimeongeza hali ambayo inamuhitaji kila mtu kushiriki katika mapambano ya kupinga hali hiyo.

"Kuna mambo ambayo hivi sasa yanaingia nchini kwetu kwa kasi hivyo kila mtu anao wajibu wa kutumia nafasi yake kupiga vita vitendo hivi ambavyo kama hatutachukua hatua za haraka tutaangamizi kizazi chetu cha sasa,"alisema.

Aidha, alishauri serikali kuacha kukubali mikopo yenye masharti ambayo yanakwenda kinyume na maadili ya kitanzania na uumbaji wa Mungu.

"Tusikubali misaada ambayo inaajenda zenye maslahi yao binafsi bora tuendelee kuwa maskini kuliko kuharibu kizazi chetu kwa kuunga mkono mambo ambayo siyo mila na desturi zetu lakini pia ni kinyume na mpango wa Mungu kwa mwanaume kumuoa mwanaume mwezake." alisema.

Aliongeza: "Kama tusipokemea na kupinga mambo haya hata sisi tutakuwa tumeshiriki katika dhambi hiyo, hivyo tutumie nafasi zetu popote tulipo makazini, kanisani kukemea kuhusu mambo haya".

Kadhalika, alisema kutokana na maendeleo ya teknolojia duniani utandawazi umekuwa ukitumika vibaya hali ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa vitendo vya mmomonyoko wa maadili.

Kutokana na hali hiyo aliiomba serikali kuweka chombo ambacho kitahakikisha mambo yaliyopo katika mitandao ya kijamii yanachujwa ili yasiwafikie watoto wadogo.

"Utandawazi ndiyo umekuwa chanzo kikubwa cha hayo yote watoto wadogo wanatumia simu na kuangalia vitu ambavyo havifai kwa rika lao, hivyo tunaiomba serikali kuona ni kwa jinsi gani kuwepo na utaratibu wa kuchuja mabaya yote ili yasiwafikie watoto.

"Lakini kama tutaacha watoto waone kila kitu kwenye mitandao tutaharibu kizazi chetu wenyewe kwakuwa wao bado hawajui kutofautisha kinachofaa kwao na kisicho faa kwao" alisema.

Paroko Msaidizi wa Parokia hiyo, Padri Paskali Dionisi, alisema kila mwanamke nchini anaowajibu wa kuhakikisha kuwa anawajibika katika malezi na makuzi ya watoto kikamilifu ili kukabili hali hiyo ya mmomonyoko wa maadili.

"Niwapongeze kinamama kwa kuandaa tamasha hili ambalo pamoja na mambo mengine wamelitumia kutoa elimu kwa jamii kupinga vitendo vya ndoa za jinsia moja pamoja na rushwa ambayo ni adui wa haki kwani watu wengi wanakosa haki zao kutokana na rushwa" alisema.

Mwenyekiti wa WAWATA Parokia hiyo, Euzebia Edward, alisema lengo la tamasha hilo ni kuelimisha jamii kuhusu vitendo mbalimbali vya mmomonyoko wa maadili ikiwemo ndoa za jinsia moja pamoja na athari za rushwa katika jamii.

## Simbachawene akimwagia 'maua' OUT kupika wahitimu

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amesema asilimia kubwa ya wahitimu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), wana uwezo mkubwa wa kuchanganua na kukabiliana na vikwazo mbalimbali vinavyokabili jamii.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza kwenye mkusanyiko wa pili wa Jumuiya ya Wahitimu wa OUT, uliofanyika katika mkoani hapa.

"Uzuri wa aliyesoma chuo hichi huwezi kumfananisha na mtu mwingine yeyote sababu huku anafundishwa kujitegemea kwa kutafuta mahitaji yote yampasayo kusoma, mazingira hayo ndio anayokutana nayo kazini, hivyo wanatengenezwa wahitimu ambao ni viongozi imara," alisisitiza.

Naye, Mbunge wa Singida Mjini ambaye pia ni Rais mpya wa jumuiya ya wahitimu wa chuo hicho, Mussa Sima, alitoa rai kwa wahitimu kushikamana ili kuchangia maboresho ya chuo.

"Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kimetusaidia sana, mtumishi aliyepo kazini badala ya kuacha kazi na kwenda kusoma, sasa ana nafasi ya kupata elimu ya chuo kikuu na bado anaendelea na majukumu ya kazi yake. Hii inamsaidia kuongeza ujuzi na kukua katika ajira kiutumishi," alisema.

Rais wa Jumuiya hiyo aliyemaliza muda wake, Almas Maige ambaye pia ni Mbunge wa Tabora Kaskazini, alisema ni wajibu kwa kila mhitimu kushiriki katika chama cha wahitimu ili kushiriki katika kutoa mchango wao wa kimawazo, kiuchumi, kijamii, utafiti na huduma za kitaalam.

Awali, Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Elifas Bisanda, alisema ni muhimu kupata taarifa za maendeleo ya elimu ya wahitimu ili kuimarisha mitaala yao.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Teknolojia za Kujifunzia na Huduma za Mikoa, Prof. Alex Makulilo, alisema chuo kinapiga hatua kubwa katika kuzalisha wataalamu wabobezi na wenye ujuzi wa kutosha wa kuwahudumia Watanzania.



# RC: Wananchi waunganishiwe maji ndani ya siku tatu

**Na Elizabeth John,** NJOMBE.

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka ametoa siku tatu kwa Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini, (RUWASA) wilayani Ludewa, kuhakikisha wanaunganisha maji kwenye mradi ulioanzishwa na wananchi katika Kijiji cha Luvuyo.

Mradi huo ulisimama ili kupisha ujenzi wa mradi mkubwa wa Igongwi ambao unapeleka maji katika Halmashauri ya Mji wa Njombe mkoani humo.

Aliitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki kwenye mkutano wa hadhara wa wananchi wa Kijiji cha Luvuyo uliofanyika Kata ya Madope wilayani Ludewa mkoani Njombe.

Mtaka alisema Kijiji cha Luvuyo tayari kina maji ya kutosha, hivyo kabla maji hayo kupelekwa sehemu nyingine mamlaka hiyo inatakiwa kuhakikisha yanapatikana kijijini hapo ndani ya siku tatu kuanzia sasa.

"Kwa sababu maji ya hapa hayahitaji miujiza kwakuwa yapo kwa wakati wote simamisha unapotaka kupeleka maji yaanze kuja kwanza hapa kwao ili wananchi waanze kutumia maji yao" alisema Mtaka.

Alisema serikali haiwezi kupuuza hisia za wananchi wa kijiji hicho kuhusu changamoto ya maji wakati uwezekano wa kupata maji upo kwakuwa wana vyanzo vya maji vya uhakika.

Meneja wa RUWASA Wilaya ya Ludewa, Jeremiah Maduhu alisema Kijiji cha Luvuyo kina mradi wa zamani wa maji ambao ulijengwa chini ya ufadhili wa Kanisa Katoliki mwaka 2012.

Alisema chanzo cha maji katika mradi huo kimejengwa pamoja na mradi mwingine wa maji wa Igongwi ambapo taharuki kwa wananchi wa kijijj hicho imekuja wakidhani huenda maji hayo yanahamishwa kupelekwa eneo lingine wakati wao hawana maji kijijini hapo.

"Baada ya kuwa changamoto imeonekana maji yakitoka kwenye chanzo ambacho kimejengwa kwa ajili ya mradi wa maji wa Igongwi kwenda Njombe chanzo cha maji ambacho kinahudumia hapa Luvuyo, maji yalikuwa hayawezi kufika kwa wananchi hivyo kusababisha changamoto ya upatikanaji wa maji," alisema Maduhu.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Luvuyo kilichopo Kata ya Madope wilayani Ludewa mkoani Njombe, Aneth Sang'anile, Nico Mgogo na Adelina Mtega waliishukuru serikali kwa kuingilia kati changamoto ya upatikanaji wa maji katika kijiji hicho ambayo ilikuwa inawasumbua kwa muda mrefu.

"Tulichangishana fedha kwa viboko na kuwekwa mahabusu ili mradi huu wa maji uweze kukamilika lakini tunashangaa kuona serikali inajenga mradi mwingine kwenye chanzo chetu cha maji kwa juu kusababisha sisi kukosa maji kabisa," alisema Mtega.

Matrida Mgimba alisema tatizo la ukosefu wa maji kijijini hapo inawaathiri hata wanafunzi wa shule kwani wanalazimika kukosa masomo kutokana na kufuata maji mtoni wakati huo vipindi vinaendelea darasani.

"Wanafunzi wananyanyasika sana kuchota maji mtoni muda wa vipindi unafika maji hayatoshi, inabidi wachaguliwe wengine wachote maji hivyo wanakosa masomo na kusababisha kuathirika kitaaluma," alisema Mgimba.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Jobee general contractors. Co. Ltd, Adam Simba ambaye anatekeleza mradi mkubwa wa Igongwi alisema wananchi wamezuia kuendelea kwa mradi huo tangu Januari mwaka huu.

# Ukarabati madarasa yaliyoteketea kwa moto waanza

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MCHAKATO wa ukarabati wa vyumba viwili vya madarasa vya Shule ya Sekondari Iyela ya jijini Mbeya ambavyo viliteketea kwa moto umeanza kufanywa na wadau, huku wazazi wakizuiwa kuchangishwa.

Mdau wa maendeleo mkoani Mbeya, Ndele Mwaselela aliahidi kushirikiana na marafiki zake kukarabati vyumba hivyo ndani ya muda mfupi ili wanafunzi wa shule hiyo waendelee kuvitumia kusoma.

Mwaselela alisema atatumia mapato yanayotokana na shule zake za Patrick Mission ya jijini Dar es salaam na Paradise Mission iliyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya pamoja na michango ya rafiki zake kukarabati madarasa hayo.

Alitoa ahadi hiyo juzi alipofanya ziara katika shule hiyo kwa lengo la kuangalia madhara yaliyojitokeza pamoja na kuzungumza na wazazi wa watoto wanaosoma kwenye shule hiyo ambapo alisema ukarabati huo utaanza hivi karibuni.

"Mimi ni mwakilishi wa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Taifa, Dk. Samia Suluhu Hassan, sasa siwezi kumwangusha hata kidogo hivi vyumba viwili tutakarabati mimi na marafiki zangu na nitasimamia ili kuhakikisha vinakamilika kwa wakati," alisema Mwaselela.

Aliwataka wazazi kuwalea watoto wao katika maadili mema ili kuepuka uharibifu wa miundombinu kama ambao ulitokea kwenye shule hiyo ambapo mmoja wa wanafunzi alianzisha moto huo.

Hata hivyo Mwaselela aliwataka wananchi wa kata hiyo kuendelea kuiunga mkono serikali kwa maelezo kuwa inatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ndani ya maeneo yao.



Mdau wa Maendeleo wa Mkoa wa Mbeya na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela (kushoto), akiwakabidhi wawakilishi wa wananchi wa Kata ya Iyela jijini Mbeya fedha kwa ajili ya chakula cha wanafunzi wa kidato cha nne wa Shule ya Sekondari Iyela ambao wamepiga kambi shuleni hapo wakijiandaa na mitihani ya mwisho. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Vituo vya kulea watoto kujengwa katika masoko

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU wa malezi ya watoto jijini Mbeya wameazimia kuanzisha vituo vya kulelea watoto umri wa chini ya miaka mitano kwenye masoko mbalimbali jijini hapa kwa lengo la kuboresha mazingira ya ukuaji wao.

Aidha, wamedai kuwa watoto wadogo wanaoshinda kwenye maeneo ya biashara hasa kwenye masoko wanatajwa kuwa kwenye hatari kiafya kutokana na mazingira ambayo wazazi wao wanafanyia biashara kutokuwa rafiki kwao.

Waliyasema hayo juzi kwenye kikao kazi kilichoandaliwa na Shirika la WeCare Foundation kikiwahusisha wadau mbalimbali kwa lengo la kuhamasisha utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM).

Wadau walioshiriki kikao kazi hicho ni pamoja na madiwani kutoka kwenye kata tano zenye masoko makubwa jijini hapa, maofisa watendaji, maofisa maendeleo ya jamii wa kata zote 36 pamoja na wenyeviti wa mitaa mitano.

Masoko yanayolengwa kuandaliwa vituo hivyo ni Soko Kuu la Mwanjelwa, Soko la Soweto, Igawilo na Sokomatola na Soko la Sido ambayo ndiyo yanakusanya watu wengi zaidi.

Diwani wa Kata ya Maendeleo lilipo Soko la Sokomatola, Issa Salimin alisema watoto wanaoshinda sokoni na wazazi wao wanakosa malezi stahiki akidai kuwa wanaathiriwa na mazingira yasiyo rafiki kwa ukuaji wao.

"Mimi nina soko hapa, ukiangalia tatizo hilo ni kubwa, utakuta mama anafanya biashara lakini mgongoni ana mtoto mchanga, ni muhimu tuwe na vituo ambavyo watoto wa wafanyabiashara watalelewa hapo kwa muda ambao wazazi watakuwa wanaendelea na biashara," Alisema Salimin.

Diwani wa Kata ya Igawilo, Hanada Mdidi aliomba halmashauri kutenga bajeti maalumu kwa ajili ya kuanzisha vituo hivyo ili kuepusha matatizo wanayokutana nayo ikiwemo kulishwa vyakula visivyostahili kwa makuzi yao.

Alisema baadhi ya wazazi wanakosa muda wa kuwaandalia chakula watoto wao hivyo kuwalisha viporo.

Akifungua kikao kazi hicho, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa aliwataka wadau kushirikiana kwa karibu kutekeleza lengo la kuwa na vituo vya watoto kwenye masoko akisema wazo hilo litaisaidia jamii kuwa na watoto wanaopata stahiki zote za malezi bora.

Malisa alisema kutokana na uzito wa wazo hilo ni muhimu wadau wakawa na wigo mpana wa utekelezaji wake ili badala ya vituo kuanzishwa kwenye masoko makubwa pekee, masoko madogo nayo yaanzishiwe ili kutoa huduma hiyo.

Mkurugenzi wa WeCare Foundation, Elizabeth Maginga alisema ni muhimu kwa viongozi kwenye ngazi za kata na mitaa kupata taarifa na uelewa sahihi juu ya PJT-MMMAM ili wasaidie wazazi na walezi kujitokeza kupata elimu ya programu hiyo.

Alisema wadau hao wanatakiwa kuhakikisha elimu inayotolewa inawafikia wananchi wote ili kurahisisha utekelezaji wake kwenye maeneo yao.



# Upimaji VVU warejea Zanzibar, vijana wamiminika vituoni

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

HUDUMA za uchunguzi wa Virusi Vya Ukimwi (VVU) katika vituo vya huduma rafiki na vituo vya afya vya serikali zimerejea, baada ya Serikali kusambaza vifaa vya uchunguzi katika vituo vyote vya afya.

Huduma hiyo awali ilikosekana visiwani Zanzibar kwa muda wa miezi mitatu kutokana na uhaba wa kifaa hicho na huduma za uchunguzi wa HIV zilisimama.

Akizungumza na waandishi wa habari kufuatia serikali kusambamba vifaa hivyo mtoa huduma katika Kituo cha Huduma Rafiki kwa Vijana Mwera Wilaya ya Magharib A Unguja, Fatma Yussuf alisema kwa sasa wanaendelea kutoa huduma ya upimaji wa VVU na mwitikio wa vijana wanaofika kupima umekua ni mkubwa.

Alisema kwa siku wanapokea wastani wa vijana watano, ndani ya miezi mitatu iliyopita vijana hao walikosekana kwa sababu kipimo hicho hakikuwepo.

Hivyo, aliishuruku serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kuhakikisha kifaa hicho cha uchunguzi kinapatikana ndani ya vituo vya huduma rafiki kwa vijana ili kuendeleza utoaji wa huduma.

"Kwa muda wa miezi mitatu huduma za chunguzi wa VVU zilisimama na vijana wakija kuangalia afya zao, lakini tulishindwa kutoa huduma hiyo kwa sababu hatukua na kipimo cha uchunguzi na vijana wengi tuliwakosa kuwafanyia uchunguzi" alisema.

Aidha aliwataka vijana kuendelea kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya kupima afya zao ili kujitambua mapema baada ya kufanyiwa uchunguzi.

Naye mtoa elimu rika wa kituo cha huduma rafiki kwa vijana katika kituo chicho, Khadija Ali Khamis alisema tangu kupokea vifaa hivyo wiki moja iliyopita vijana wamehamasika kupata huduma ya upimaji na ushauri nasaha sambamba na kupata huduma nyingine zinazotolewa kituoni hapo.

Aidha, aliiomba Serikali kupitia Wizara ya Afya kuweka utaratibu maalum wa kufikisha vifaa hivyo kabla ya kumalizika vituoni ili huduma za upimaji wa VVVU ziwe endelevu na vijana waendelee kuvitumia vituo hivyo.

Baadhi ya vijana wanaotumia kituo hicho cha huduma rafiki Mwera, walisema kupatikana kwa kifaa hicho cha uchunguzi wa VVU kitaongeza ushawishi wa kupima afya zao kwa sababu ilipokuwa huduma hiyo haipatikana hulazimika kwenda katika vituo vya afya binafsi ambapo huduma hiyo hulipia.

"Katika vituo vya huduma rafiki na vituo vya afya vya serikali huduma hii hupatikana bure lakini katika vituo binafsi unalipia" alisema Juma Said kijana alieyefika kituoni hapo.

Naye, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema tatizo la uhaba wa kifaa hicho kulitokana na kuchelewa kufika kwa meli iliyokuwa imebeba vifaa hivyo ambapo Serikali ya Zanzibar inapata msaada kutoka Global Fund.

Alisema vifaa vilivyopo kwa sasa vitakidhi mahitaji kwa muda wa mwaka mmoja na tatizo la uhaba wa vifaa hivyo halitajirejea.

Alisema: "Tumefurahi kuona hamasa ya wananchi hasa vijana kupima afya zao kuchunguza VVU zimeongezeka, niwaombe kuendelea kujitokeza kwa wingi kujua afya zao vifaa vya uchunguzi sasa vipo vya kutosha".



Baadhi ya wananchi wa kijiji cha Matemwe Mkoa wa Kaskazini Unguja wakiwa katika mkutano wa kueleza changamoto zinazowakabili katika vijiji vyao mkutano ambao umeandaliwa na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mahmoud. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Walalamika kutoajiriwa katika hoteli zilizopo kijijini kwao

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WANANCHI wa Kijiji cha Kijini na Mbuyu Tende Jimbo la Matemwe Mkoa wa Kaskazini Unguja wamesema wamechoka kudanganywa kuhusu kupatiwa ajira katika hoteli zilizopo kijiji hapo.

Walisema licha ya kuwa vijiji hivyo vimezungukwa na hoteli nyingi za kitalii na kuahidiwa ajira lakini wanaonufaika ni wageni kutoka nje ya vijiji hivyo.

Walieleza kero hiyo wakati wa mkutano uliowashirikisha wananchi wa vijiji hivyo na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja Ayoub Muhammed Mahmoud, ikiwa ni mwendelezo wake wa kusikiliza kero za wananchi.

Wananchi hao walisema kwa sasa wanamaisha magumu kunakosababishwa na ukosefu wa ajira.

Haji Ali Mcha, alisema hoteli zilizopo katika vijiji hivyo hakuna mwananchi hata mmoja kutoka katika vijiji vyao walipewa ajira, licha ya kuahidiwa na serikali ya mkoa huo kuwa wananchi wazawa ndio watakaopewa kipaumbele katika kupata ajira.

"Waheshimiwa mnatupoteza, wakati hoteli zinajengwa hapa mlituahidi kuwa mtatupatia ajira katika hoteli hizo, lakini tunashangaa kuona hakuna mwananchi wa Kijiji cha Kijini wala Mbuyu Tende alienufaika na ajira hizo.

Lakini tunawaambia kuwa Uchaguzi Mkuu kesho kutwa tukutane mwaka 2025" alisema.

Alisema wananchi wa vijiji hivyo wanakabiliwa na tatizo la njaa kunasababishwa na hali duni ya maisha.

Mkuu wa Mkoa huo, Ayoub Muhammed Mahmoud akijibu hoja hiyo alisema, wakati ujezi wa hoteli moja kijijini hapo Serikali ya Mkoa iliomba ajira kwa wananchi wa kijiji hicho lakini nafasi hizo hazijapatikana.

Alisema dhana ya upatikanaji wa ajira katika hoteli za kitalii kuna haja ya kupitiwa upya kwa sababu wananchi wa vijiji husika hawapati fursa za ajira.

Alisema: "Tutashirikiana na masheha ili kupitia hoteli kwa hoteli kujua wafanyakazi waliopo na wangapi kutoka katika vijiji husika na katika hili serikali kuu imeliona muda si mrefu itapitishwa sheria kila mwenye hoteli lazima kuajiri wafanyakazi kutoka sehemu husika".

# Serikali kujenga vituo vya ufundi Unguja, Pemba

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanza mchakato wa ujenzi wa vituo vya mafunzo ya amali (ufundi) vitakavyojengwa Unguja na Pemba ili kuwasaidia wanafunzi watakaokosa sifa za kujiunga na elimu ya juu kujiendeleza na kupata ujuzi.

Makamu wa Pili wa Rais Hemed Suleiman Abdulla aliyasema hayo wakati akihutubia katika kilele cha Maadhimisho ya Miaka 59 ya Elimu Bila Malipo Kisiwani Pemba.

Alisema Serikali imekusudia kujenga vituo vitano vya mafunzo ya amali sambamba na kujenga Chuo cha Ubaharia katika eneo la Bait el Ras Zanzibar.

Hemed alisema kuwa Serikali ya Zanzibar inaendelea na hatua za upatikanaji wa vifaa vinavyohitajika katika kujifunza na kufundishia, kuzindua mradi mkubwa wa kuimarisha ubora wa elimu ya lazima.

Aidha, alisema kuwa miongoni mwa matunda ya mapinduzi ya mwaka 1964 ni kuondoa ubaguzi na kuleta usawa katika upatikanaji wa elimu kwa wote bila ya kujali itikadi, rangi, kabila, dini na uwezo wa kiuchumi.

Hata hivyo alisema kwa mwaka wa fedha 2023- 2024 Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imejipanga kujenga Shule 26 za ghorofa kwa Unguja na Pemba.

Alisema shule hizo zitatatua changamoto ya uhaba wa madarasa, msongamano wa wanafunzi hasa katika visiwa vidogo vya Tumbatu na Kojani.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa alisema kuwa serikali imeipa kipaumbele sekta ya elimu kwa kutenga fedha nyingi ili wanafunzi wapate elimu bora kwenye mazingira mazuri.

Alisema wizara itahakikisha pamoja na kusimamia kila mtoto anapata elimu ya lazima bure na katika mazingira wezeshi, pamoja na kuwataka wazazi, walezi, wanafunzi na walimu kuthamini juhudi hizo kwa kuongeza ushirikiano na kusoma kwa bidii ili kupata matokeo mazuri yatakayoakisi dhamira ya Mapinduzi ya Zanzibar kufuta ujinga na dhuluma.

Katibu Mkuu Wizara hiyo, Khamis Abdallah Said alisema kuwa tamasha la elimu bila ya malipo limejumuisha michezo mbalimbali, lengo ni kuibua vipaji kwa wanafunzi.

# Wenye ulemavu walalamikia mamlaka kuwakosesha haki

**Na Thobias Mwanakatwe,**

SINGIDA

WATU wenye ulemavu mkoani hapa wamezilaumu serikali za mitaa kwa kutowashirishika kwenye mipango ya maendeleo kwa madai kuwa ni wasumbufu, jambo linalowakosesha haki za kiuchumi.

Ni malalamiko waliyoyatoa wakati wa uzinduzi wa mradi wa uongozi na haki za kiuchumi kwa wanawake utakaotekelezwa mkoani hapa kwa ubia wa Shirika la UN Women na Shirika la Maendeleo ya Jamii la TUSONGE kwa ufadhili wa Serikali ya Finland.

"Viongozi wa serikali za mitaa wamekuwa hawawashirikishi watu wenye ulemavu kwenye mipango ya maendeleo, wanawatenga," alidai Ziada Nsembo, mwenye ualbino.

Rehema Hassan alisema serikali za mitaa haziwashirikishi walemavu katika mipango ya maendeleo kutokana na dhana potofu iliyojengeka katika jamii kuwa ni wabishi kwa kuwa wamekuwa wakihoji mambo mengi kwenye vikao na mikutano.

Rehema alitoa ushuhuda wa jinsi unyanyasaji aliodai unafanywa kwa wanafunzi wenye ulemavu katika shule iliyoko Manispaa ya Singida.

Alisema katika shule hiyo, mwalimu alimtoa mwanafunzi huyo kukaa mbele darasani na kumpeleka nyuma. Alidai baadaye mwanafunzi huyo alimua kuhamia shule nyingine iliyoko wilayani Ikungi ili kuondokana na fedheha.

Husna Abdallah, alisema wakati anasoma katika shule moja, mkuu wa shule hiyo ya sekondari iliyoko wilayani Mkalama aliwadharau wanafunzi wenye ualbino kwa kuwatamkia kuwa wamelaaniwa, hali iliyosababisha 11 kususa kula chakula cha shuleni.

Ziada Nsembo, alidai mwaka 2005 wakati kulipokuwa na matukio mengi ya kufukua makaburi yanayosadikiwa kuzikwa watu wenye ualbino, mtoto wake alipofariki dunia alipokwenda kumzika, alilazimika kuandika jina tofauti na alilokuwa anafahamika kwa hofu kaburi lake kufukuliwa na kuchukuliwa viungo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TUSONGE, Aginatha Rutazaa, alisema wanawake wakishirikishwa kwenye uamuzi kuanzia ngazi za chini kutasaidia kuleta sera zenye kuheshimu usawa wa kijinsia katika jamii ya Kitanzania.

"Serikali za mitaa ndiko chimbuko la mifumo dume kandamizi ambayo inatokana na mila na desturi, hivyo TUSONGE itafanya kila jitihada kupambana na changamoto hiyo ili kuwe na usawa na idadi kubwa ya wanawake waweze kushiriki kwenye uongozi," alisema.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Kasulu, Theresia Mtwele, akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa tawi la BRAC wilayani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara wa Tanzania, Afrika Kusini wateta uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA wa Tanzania wameteta na wenzao kutoka Afrika Kusini katika mkutano wa Jukwaa la Wafanyabiashara uliofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Mkutano huo pia ulihudhuriwa na Balozi wa Afrika Kusini nchini Noluthando Malepe.

Wakati wa mkutano huo, Balozi Noluthando Malepe aliitaja Tanzania kama moja ya nchi bora zaidi kwa uwekezaji kutokana na kuwapo fursa nyingi za kibiashara.

Alitaja kuwapo amani nchini na ushirikiano wa kihistoria uliodumu kwa muda mrefu baina ya Tanzania na Afrika Kusini kama nguzo muhimu katika kufanikisha ustawi wa biashara baina ya mataifa hayo mawili.

"Hivyo, ninawaomba sana itumieni vyema fursa hii ya amani na ushirikiano tuliona nao na wenzetu wa Tanzania kustawisha biashara zenu. Kokote mnapohisi kuna changamoto tunawakaribisha ofisi za ubalozi ili tuweze kujadili namna bora ya kuzitatua huku pia tukijadili fursa nyingine zaidi,'" aliomba Balozi Malepe.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wafanyabiashara wa Afrika Kusini nchini, Manish Thakrar alisema pamoja na mambo mengine, nia ya jukwaa hilo ni kuunga mkono jitihada za serikali katika kuvutia wawekezaji wengi zaidi kutoka nje ya nchi kuja kuwekeza nchini.

Alitaja suala la upatikanaji huduma za kifedha za uhakika kama moja ya nguzo muhimu katika kufanikisha ajenda hiyo.

"Habari njema ni kwamba ushirikiano wetu na benki ya NBC uliodumu kwa muda mrefu sasa umeendelea kutuhakikishia upatikanaji wa huduma bora za kifedha.

"Tumefarijika zaidi kusikia kwamba NBC wanaendelea kutuhamasisha kuhusu ushiriki wetu kwenye soko la G-20 huku wakituhakikishia ufanisi zaidi kwenye upatikanaji wa mitaji zaidi na huduma nyingine nyingi za kifedha," alisema Thakrar ambaye pia alionyesha kuvutiwa zaidi na huduma ya malipo ya mtandao ya NBC Connect.

Awali, uongozi wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) ulisisitiza kuhusu dhamira yake ya kufanikisha ustawi wa biashara baina ya Tanzania na Afrika Kusini kwa kuwawezesha wafanyabiashara wa mataifa hayo mawili ili wapanue zaidi biashara zao sambamba na kuchangamkia fursa zaidi nje ya mipaka ya nchi hizo.

Hiyo inatokana na hatua ya Umoja wa Afrika (AU) kujumuishwa kuwa mwanachama wa kudumu katika muungano wa G-20.

Mkurugenzi wa Hazina na Masoko ya Fedha wa Benki ya NBC, Peter Nalitolela, alieleza hayo kwa wafanyabiashara hao alipozungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Theobald Sabi.

Kwa mujibu wa Nalitolela, kupitia huduma zake mbalimbali za kifedha ikiwamo mikopo ya ukuzaji mitaji, dhamana, huduma ya fedha za kigeni sambamba na huduma ya malipo kwa njia ya mtandao, benki hiyo imedhamiria kurahisisha zaidi ufanisi wa biashara kwa wafanyabiashara wa mataifa hayo ili washiriki kwa ushindani zaidi kwenye fursa hiyo mpya ya kimataifa.

"Tumefurahi kuona kwamba Mheshimiwa Balozi wa Afrika Kusini hapa Tanzania, Noluthando Malepe naye amewasisitiza wafanyabiashara kuchangamkia soko hili jipya la G-20.

# Balozi UN kusaidia familia duni na jamii ya wafugaji

**Na Salome Kitomari**

BALOZI wa Umoja wa Mataifa (UN) Tanzania, Ami Inbar ameeleza nia yake ya kuendelea kusaidia familia duni na jamii za wafugaji kubadili maisha yao kiuchumi.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa njia ya mtandao, balozi huyo ambaye anafahamika kwa kuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Milenia (SDG), alisema matamanio yake ni kuona watu wa familia duni, maisha yao yanabadilika.

Balozi Inbar ambaye ni mwanzilishi wa mfuko wa kusaidia jamii wa Nau Charitable Fund na mwenye mchango mkubwa kwenye kulinda utambulisho wa pekee wa nchi, alisema mara zote alipokuwa Tanzania ameshirikiana na jamii za wafugaji ya Maasai kwenye shughuli za uzalishaji.

Alisema kutokana na kazi hizo ameshirikiana na taasisi nyingine kama Marvelous Foundation ya New York, Marekani na pia amefika nchi za Ukraine, Israeli, Ugiriki na Dubai.

Taasisi hiyo inatekeleza miradi mbalimbali ya kuwezesha jamii nchi za Tanzania na Kenya kupata chakula, elimu na huduma za afya kwa watoto wenye uhitaji na watu wazima.

Alisema kuwa yeye na wenzake wanawasaidia watoto kutoka familia za mzazi mmoja kupata mahitaji yote ya elimu ikiwamo kulipa ada katika Shule ya O'Brien iliyoko katikati ya Moshi na Arusha ambayo ni kwa ajili ya watoto wa jamii ya kimasai.

"Kutokana na msaada wetu tumerudisha tabasamu kwa watoto hawa ambao sasa wanaendeleo na masomo, wanatoka familia duni ambazo ni za mzazi mmoja na walikuwa nyumbani kwa sababu walikosa ada.

"Ni muhimu sana kuwapa elimu kwa ajili ya maisha yao ya baadaye, shuleni wanapewa sare za shule, viatu na chakula. Lakini walikosa ada, hivyo tumewawezesha kuendelea na masomo bila kikwazo chochote," alisema.

Kwa mujibu wa Inbar, alihamaisha wenzake ambao walikwenda mkoani Arusha na kukutana na jamii ya kimasai ambao waliwaeleza changamoto zao ni ukosefu wa maji, chakula, dawa na huduma za mifugo.

"Tumepeleka misaada muhimu kama dawa, chakula, vinywaji na tumenunua ng'ombe 200 wakati huo na tuna mpango kuongeza ili kuwawezesha kupata maziwa na mazao mengineyo ya mifugo. Kwa kweli tulikutana na wahitaji wengi sana, hivyo tumeweka mkakati wa kuwasaidia kupunguza changamoto zinazowakabili," alisema.

## Marekani kuipiga jeki Kenya kurejesha utulivu Haiti

**WASHINGTON,** Marekani

SERIKALI ya Rais wa Marekani, Joe Biden, ameahidi msaada wa Dola milioni 100 kupiga jeki juhudi ya Kenya kuongoza kikosi cha kimataifa kurejesha hali ya usalama nchini Haiti.

Hayo yalibainishwa jana, huku Washington ikitoa wito kwa mataifa mengine kuunga mkono Kenya katika juhudi zake za kukabiliana na makundi ya magenge yanayoendelea kutatiza usalama wa raia katika taifa hilo la Haiti.

Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Marekani Antony Blinken, alithibitisha kuwa Washington itatoa msaada wa usafiri, intelijensia, matibabu na mawasiliano kwa ujumbe huo wa walinda amani. Na kwamba mpango huo unafaa kuidhinishwa na baraza la usalama katika Umoja wa Mataifa (UN).

Ilibainishwa kuwa kando ya Kenya ambayo itaoongoza ujumbe huo, mataifa mengine kama Jamaica, Bahamas, Antigua na Barbuda yameahidi kuwatuma wanajeshi wake.

Rais wa Kenya William Ruto, alisema nchi yake imejitolea kuongoza kikosi cha kimataifa cha walinda amani nchini Haiti kama njia moja ya kurejesha hali ya utulivu na mpangilio kwenye taifa hilo.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa zaidi ya watu 20,000, raia wa Haiti, wanaishi katika makazi duni ya muda baada ya kutoroka makazi yao kutokana na mashambulizi ya magenge yenye silaha.

Magenge hayo pia yameripotiwa kuteka barabara muhimu kaskazini na kusini mwa Haiti, hali ambayo imetatiza usambazaji wa chakula. Vile vile, zaidi ya watu milioni nne nchini Haiti wanakabiliwa na tatizo la baa la njaa, huku milioni 1.4 wakiwa katika hatari kubwa. **RFI**

## Viongozi mapinduzi Niger waishutumu UN

**NIAMEY,** Niger

VIONGOZI wa mapinduzi wa Niger wamemshtumu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Atonio Guterres kwa madai ya kukwamisha ushiriki wao katika Baraza Kuu la taasisi hiyo, wakisema hatua hiyo inakwamisha juhudi zozote za kumaliza mzozo huo katika nchi yao.

Viongozi hao walitoa tuhuma hizo mwishoni mwa juma lililopita, na kwamba mashauriano ya kurejesha utawala wa kiraia bado hayajazaa matunda, huku utawala wa kijeshi ukitaka kipindi cha mpito cha miaka mitatu na Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS) ikitoa wito wa kurejeshwa mara moja rais aliyechaguliwa kidemokrasia.

Mapinduzi hayo pia yalikosolewa vikali na serikali za Magharibi na mashirika ya kimataifa kama vile UN ambayo inasimamia Mkutano Mkuu wa viongozi wa ulimwengu huko New York Marekani.

Wakati huo huo pembeni ya mkutano huo wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, mkuu wa Mpango wa Mazingira wa umoja huo Inger Andersen, alisema uzalishaji wataka za plastiki unaongezeka duniani kote na kusababisha uchafuzi zaidi wa mazingira.

Pia Andersen alitoa wito kwa ulimwengu kufikiria upya kuhusu jinsi binadamu anavyotumia plastiki.

Ilibainishwa kuwa katika kipindi cha wiki nzima wakati mikutano inapoendelea, waandamanaji walikusanyika kwenye eneo hilo la mkutano lililowekewa vizuizi kupaza sauti zao kuhusu dhuluma katika nchi zao. **VOA/DW**



Mkutano wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN), ukiendelea New York nchini Marekani. **PICHA: MTANDAO**

# Dhamira ya Rais Samia kuvutia wawekezaji yaundiwa mkakati

**LONDON,** Uingereza

KATIKA jitihada za kuchochea mchango wa sekta ya benki Tanzania na kuimarisha ustawi wa kiuchumi wa taifa, Abdulmajid Nsekela, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki la CRDB, yuko Uingereza katika ziara inayolenga kukuza ushirikiano wa kimkakati wa benki hiyo na kuvutia uwekezaji wa kigeni Tanzania kutoka jukwaa la kimataifa.

Hatua hii ya kimkakati inakwenda sambamba na hatua zinazochukuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan katika kujenga mazingira mazuri na ya kuvutia wawekezaji kuja kuwekeza Tanzania.

Jitihada za Nsekela zinalenga kushawishi wawekezaji wa kimataifa wanaotaka kuingia katika masoko yanayochipukia kama vile Tanzania.

Katika ziara hiyo amekutana na kufanya mazungumzo na wawekezaji, benki za biashara na taasisi za fedha za maendeleo kutoka nchi na ukanda tofauti duniani, ikiwa ni pamoja na Uingereza, Marekani, Ulaya, Mashariki ya Kati na Afrika.

Mikutano hiyo ya kimkakati iliyoandaliwa kwa kushirikiana na washirika wa kimkakati wa Benki ya CRDB kimataifa ikiwamo JP Morgan, Afrieximbank, na Standard Bank, imejumuisha mada mbalimbali kuanzia fursa za uwekezaji nchini Tanzania, ufadhili endelevu na ubunifu, kukuza biashara ndani ya Afrika na kuchochea ujumuishi wa kifedha hasa kupitia taasisi yake ya CRDB Bank Foundation.

Nsekela anaamini kwamba sera rafiki za uwekezaji nchini, hali ya amani na utulivu, uwezo mkubwa wa kustahimili deni na viwango thabiti vya mfumuko wa bei, vinaifanya Tanzania kuwa sehemu inayovutia kwa wawekezaji.

Takwimu za hivi karibuni kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) zinaonesha mwezi Agosti 2023 pekee, miradi 58 ya uwekezaji imesajiliwa, yenye thamani ya jumla ya Dola za Marekani bilioni 931.6.

"Miradi hii ina uwezo wa kutoa nafasi za ajira 25,731 katika sekta mbalimbali kama vile uzalishaji, usafirishaji, kilimo, utalii, ujenzi wa biashara, huduma na miundombinu ya kiuchumi.

"Uwekezaji wa Moja kwa Moja wa Kigeni (FDIs) unachangia kwa kiasi kikubwa katika miradi hii, jambo linaloonesha imani kubwa yawawekezaji wa kimataifa kwa Tanzania," alisema.

Alibainisha kuwa mwaka 2022, Benki ya CRDB ilikuza ushirikiano wake wa kimataifa na taasisi mbalimbali duniani kama Proparco, USAID, DFC, na IFC, na kupata zaidi ya Sh. bilioni 500 kusaidia wajasiriamali wadogo na wa kati.

Mafanikio haya yanathibitisha imani na nafasi ya Benki ya CRDB kimataifa na utayari wake wa katika kusaidia kuimarisha na kukuza ustawi wa kiuchumi, hasa wakati wa kipindi kigumu cha janga la UVIKO-19.

Nsekela alisema "Uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika katika nyanja zote ikiwamo sekta za biashara na viwanda, na hivyo kuifanya kuwa fursa nzuri kwa wawekezaji wa ndani na wa nje."

Nsekela alipongeza mageuzi makubwa yaliyotekelezwa na Rais Samia, yamesaidia kuboresha sana mazingira ya biashara nchini na hivyo kuvutia wawekezaji wengi.

Alibainisha kuwa mafanikio ya mikutano hiyo na wawekezaji yanachangiwa na mageuzi yaliyofanywa na Serikali ambayo yamerudisha imani ya wawekezaji wengi kwa Tanzania.

ALIsema, "Dhamira iliyodhihirishwa na Rais wetu imeweka njia kwa mikutano muhimu hii. Lengo letu kuu katika mikutano hii ni kuonesha utajiri wa fursa zinazowasubiri wawekezaji katika nchi yetu. Zaidi ya hayo, tunawahakikishia msaada wetu wa kifedha, ukiwa na bidhaa na huduma zetu za ubunifu, ili kuhakikisha uendeshaji mzuri wa shughuli zao wanapokuja kuwekeza nchini."

Nsekela alisisitiza kwamba kwa wawekezaji wanaotaka kufanya kazi katika eneo la Afrika Mashariki na zaidi, Benki ya CRDB kwa sasa inafanya kazi Tanzania, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Mtandao huu wa kikanda, pamoja na mkakati wake wa upanuzi wa siku zijazo, unaiweka benki hiyo katika nafasi nzuri ya kusaidia ajenda ya kukuza biashara ndani ya Afrika.

Benki ya CRDB ikiwa kinara wa ufadhili endelevu unaozingatia utunzaji wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, Ofisa Mtendaji Mkuu wake, Nsekela, na ujumbe wake pia walifanya mazungumzo na wawekezaji wa kimkakati katika hatifungani ya kijani ya kwanza nchini na kubwa zaidi ukanda wa Jangwa la Sahara iliyotolewa hivi karibuni na benki hiyo, "Kijani Bond."

Hatifungani hiyo ni sehemu ya Programu ya Hatifungani ya Muda wa Kati ya Benki ya CRDB yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 300, inalenga kukusanya Sh. bilioni 40 na nyongeza ya hadi Sh. bilioni 15.

Nsekela alifichua kwamba tangu kufunguliwa dirisha la uwekezaji mnamo tarehe 31 Agosti 2023, idadi kubwa ya wawekezaji wameonesha nia ya kuwekeza katika Kijani Bond.

"Kuna wawekezaji wengi wa ndani na wa kimataifa waliojitokeza kuwekeza katika Kijani Bond. Shirika la ya Fedha la Kimataifa (IFC), liimejitolea kuwekeza asilimia 40 katika Kijani Bond," alibainisha.

Aliwasihi watu binafsi kutumia fursa ya kuwekeza katika Kijani Bond, kwani kuna wiki chache tu kabla ya dirisha la uwekezaji kufungwa tarehe 6 Oktoba 2023.

"Kwa uwekezaji wa kuanzia Sh. 500,000 na viwango vya riba kinavyovutia cha asilimia 10.25, hatifungani hii inatoa fursa ya kukuza kipato na kusaidia utekelezaji wa ajenda ya maendeleo ya nchi," alisema.

Ikianzishwa mwaka 1996 na baadaye kuorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) mwaka 2009, Benki ya CRDB imekuwa kinara katika sekta ya benki nchini Tanzania kwa zaidi ya miaka 27, ikipata mafanikio mengi. Ni ya kwanza nchini kuendesha kampuni ya bima, CRDB Insurance Company Ltd, inayotoa huduma za bima za jumla.

# SERENGETI GIRLS YAONA UDHAIFU, KUJIPIMA TENA NA MOROCCO

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Timu ya Tanzania ya Wasichana chini ya miaka 17 ('Serengeti Girls'), Esther Chabruma, amesema mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Morocco juzi, imekuwa kipimo kizuri kwao kuandaa timu kuelekea michezo ya kuwania nafasi ya kushiriki fainali za Afrika na Kombe la Dunia.

Serengeti Girls ambayo leo itarudiana tena na Wamorocco hao, juzi iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 katika mchezo wa kirafiki uliopigwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, mabao ya Tanzania yakifungwa na Masika Khing na Sabina Alex huku la wapinzani wao likikwamishwa nyavuni na Bentahri Ouafa.

Akizungumza juzi baada ya kukamilika kwa dakika 90 za mchezo huo wa kirafiki, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Chabruma, alisema mechi hiyo imewasaidia kuona ni wapi wanatakiwa kufanya marekebisho kulingana na changamoto walizoziona katika mchezo huo.

Aliwapongeza wachezaji wake kwa kucheza vizuri na kushinda mchezo huo, lakini akisema kikubwa kwake ni kuona vijana hao wamefuata kile alichowaambia katika uwanja wa mazoezi na kukitekeleza katika mechi hiyo.

> **"Kuna vitu sisi kama benchi la ufundi tumeviona, ubora wa wachezaji wetu na wapi pa kuongeza nguvu ili kuwa bora zaidi.**

"Morocco wamekuwa kipimo kizuri kwetu ukizingatia wachezaji niliokuwa nao wengi wametoka ligi ya chini (mkoa) hakuna mwenye uzoefu wa kucheza mechi kubwa kama hii," alisema Chabruma.

Aliongeza kuwa anaamini makosa yao watayafanyia kazi kwa sababu watakuwa na mchezo wa marudiano dhidi ya Morocco leo kuendelea kujipima tena na kuwapa vijana uzoefu kwa kucheza mechi za ushindi.

Serengeti Girls itashuka tena Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, leo Saa 10:00 alasiri kucheza mchezo wa marudiano dhidi ya mabinti hao wa Morocco waliopo hapa nchini kwa mechi hizo za kirafiki.



Msanii wa Bongo Fleva, Salmin Ismail maarufu Kusah, akitumbuiza kwenye mahafali ya Shule ya Msingi na Sekondari ya Green Acres, Mbezi Beach Salasala, Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# *Msanii Kusah ataka shule ziibue vipaji*

**Na Joseph Mwendapole**

MSANII wa Bongo Fleva, Salmin Ismail maarufu Kusah, amezitaka shule nchini kutenga muda wa kutosha wa michezo ili waweze kuibua vipaji mbalimbali vya wanafunzi.

Kusah aliyasema hayo mwishoni mwa wiki baada ya kutumbuiza kwenye Mahafali ya 23 ya Shule ya Awali, Msingi na Sekondari ya Green Acres ya Mbezi Beach Salasala, Dar es Salaam.

Alisema sanaa ni muhimu kwani baadhi ya watu duniani wamefanikiwa kuwa maarufu na kupata utajiri mkubwa kutokana na vipaji vyao vya muziki, mpira, kuogelea na michezo mbalimbali.

"Kuna mwanafunzi mwingine anaweza asiwe vizuri sana darasani, lakini akawa mzuri sana kwenye kuimba au kucheza mpira, kwa hiyo lazima kipaji chake kiibuliwe mapema na kukuzwa kwa sababu unaweza kukuta hiyo ndiyo thawabu yake aliyopewa na Mungu," alisema na kuongeza:

"Kuna wanafunzi ni wazuri sana kwenye masomo ya kawaida, tuwaache waendelee na mkondo huo, lakini si lazima kila mwanafunzi aende kwenye mkondo wa masomo kuna wengine kama sisi tumebahatika vipaji vya kuimba tu na tunavitumia kuishi."

Kusah alisema yeye binafsi hakufanikiwa kufika mbali kimasomo, lakini baada ya kubaini ana kipaji cha kuimba alifanikiwa kukiendeleza na kwa sasa ndicho kinamsaidia kuendeleza maisha yake kwa ujumla.

"Haiwezekani wanafunzi wote waje kuwa wahandisi, wanasheria, wahasibu kuna wengine vipaji vyao vitajieleza kwenye mpira wa miguu, muziki kama mimi, maigizo na kadhalika, kwa hiyo serikali na wadau wengine tuweke umuhimu kwenye kuendeleza vipaji vya wanafunzi," alisema

Mkuu wa shule hiyo, Minani Kafugugu, alisema shule yake imeendelea kuipa michezo kipaumbele ili kuibua vipaji vya wanafunzi shuleni hapo.

"Sisi Green Acres tumekuwa tukifanya vizuri kitaaluma, lakini tukaona tuipe michezo nayo kipaumbele kwa sababu kuna mwanafunzi anaweza kuwa na kipaji ambacho akikitumia kitamsaidia kuwa mashuhuri na kuingiza kipato kupitia kipaji chake," alisema.

Alizitaka shule mbalimbali nchini kutenga muda wa michezo kwa ajili ya kuibua vipaji vya watoto na vile vile michezo huwafanya wanafunzi kupumzisha akili zao baada ya muda mwingi wa masomo.

## Hard Rock ulimi nje Ligi Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Hard Rock imeendelea kupata matokeo mabaya katika michezo yake ya Ligi Kuu Zanzibar inayoendelea visiwani hapa baada ya hapo juzi kupokea kichapo cha mabao 3-1 dhidi ya wanajeshi wenzao wa Kipanga FC.

Hard Rock inaburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo kwa kuwa na alama moja katika michezo mitatu iliyocheza.

Miamba hiyo ya Jeshi yenye makazi yake kisiwani Pemba katika michezo mitatu imefungwa miwili na kutoka sare mchezo mmoja.

Akizungumza na Nipashe juzi, Kocha msaidizi wa timu hiyo, Vua Silima Juma, alisema kupata matokeo hayo mabaya katika michezo mitatu ya mwanzo wa ligi kumetokana na ugeni wa wachezaji wake.

Alisema wachezaji watatu tu ndio wana uzoefu katika Ligi Kuu ya Zanzibar huku wengine hii ikiwa ni mara yao ya kwanza kucheza ligi hiyo hivyo kunawafanya kuwa na hofu ya mchezo.

"Nina kikosi chenye wachezaji wazuri na vijana, lakini changamoto kubwa ni uwoga walio nao hasa hawa ambao hawajawahi kicheza Ligi Kuu, hivyo tutajipanga mchezo wetu ujao kufanyia kazi mambo ambayo tumeyaona katika michezo hii mitatu," alisema.

## Mbeya Kwanza FC yaishusha Mbeya City

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mbeya Kwanza imekwea kwenye kilele cha msimamo wa Ligi ya Championship kwa mara ya kwanza, baada ya kuwatwanga wapinzani wao wakubwa Mbeya City mabao 4-0 katika mechi ya iliyopigwa juzi Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara.

Mechi hiyo ya dabi iliyochezwa nje jiji la Mbeya imetokana na Mbeya Kwanza kuamua kuutumia uwanja huo uliopo Mtwara kama wake wa nyumbani kama ilivyokuwa wakati ipo Ligi Kuu ilipoutumia Uwanja wa Majimaji, Songea mkoani Ruvuma.

Ushindi huo umewafanya Mbeya Kwanza kuua ndege wawili kwa jiwe moja, kwanza kupata ushindi dhidi ya wapinzani wao, lakini kupindua meza kibabe kwa kuwashusha juu ya msimamo wa Ligi ya Championship ambapo kabla hapo, Mbeya City ilikuwa inaongoza kwa pointi tisa.

Mbeya Kwanza iliyoshuka daraja kutoka Ligi Kuu msimu wa 2021/22 ilipata bao la kwanza dakika ya 33 lililowekwa wavuni na Ramadhani Kapera, kabla ya Chunga Zito kupachika bao la pili kwa mkwaju wa penalti dakika ya 42.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### KUONDOKA BRENTFORD

MSHAMBULIAJI wa England, Ivan Toney yuko tayari kuondoka Brentford Januari. Klabu hiyo iko tayari kuruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ambaye anatumikia marufuku ya miezi nane kwa kukiuka sheria za kamari za FA aondoke ikiwa ada ya pauni milioni 60 itafikiwa. ***(Sunday Mirror)***

### DEMBELE AWINDWA ARSENAL

ARSENAL, Tottenham na West Ham zote zinafuatilia uwezekano wa kumnunua winga wa Paris St-Germain na Ufaransa, Ousmane Dembele kwa mkopo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alijiunga na mabingwa hao wa Ufaransa msimu wa majira ya joto akitokea Barcelona. ***(Sunday Mirror)***

### GUIMARES MKATABA MPYA

KIUNGO wa kati wa Newcastle United na Brazil, Bruno Guimaraes, amekubali kwa mdomo kuongezewa mkataba mpya huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, akipanga kuongeza mkataba wake wa sasa hadi 2028. ***(Sky Sports)***

### MAN UNITED NA HOJLUND

MANCHESTER United ilijaribu kubadilishana wachezaji kadhaa, akiwamo kiungo wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek, 26 na kiungo wa kati wa Brazil, Fred mwenye miaka 30 kama njia ya kufidia gharama ya kumsajili Rasmus Hojlund. Lakini Atalanta walikuwa wakitaka fedha taslimu kwa raia huyo wa Denmark mwenye umri wa miaka 20. ***(The Athletic)***

### ATAKIWA VILLARREAL

MCHEZAJI Donny van de Beek anawindwa na Villarreal baada ya kukosa nafasi ya kucheza pale Manchester United. ***(Fichajes)***

### MEJBRI KUFUNGWA UNITED

KLABU ya Manchester United pia imeanza mazungumzo na kiungo wa kati wa Tunisia, Hannibal Mejbri, 20, kuhusu mkataba mpya. ***(Sunday Express)***

### LEVY KUUZA HISA

MWENYEKITI wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy, yuko tayari kuuza hisa hadi asilimia 25 katika klabu hiyo. ***(Sunday Times)***

### DELE, EVERTON KUJADILI

KLABU ya Everton itajaribu kujadili upya masharti ya uhamisho wa kiungo wa kati wa England, Dele Alli, 27, kutoka Tottenham Hotspur huku wakitarajiwa kupokea pauni milioni 10 atakaposhiriki mechi zaidi ya 20 za Everton. Lakini hali ya kifedha ya 'Toffees' hao inaweza kuwalazimisha kufanya mazungumzo. ***(Sunday Express)***

### WEST BROM KUUZWA

KLABU ya West Brom imeripotiwa kuongeza kasi ya kutafuta mmiliki mpya, huku mfanyabiashara Mchina Guochuan Lai akitaka kuiuza kabla ya mwisho wa mwaka huu. ***(Mail on Sunday)***

### RAMSDALE KUUZWA

CHELSEA na Bayern Munich zimebakia kuwa na nia ya kumsajili mlinda lango wa England na Arsenal, Aaron Ramsdale, 25, ambaye amepoteza nafasi yake kama namba moja wa 'Washikabunduki' hao. ***(Mail on Sunday)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RODRI AMTIBUA PEP

**MANCHESTER,** England

**Sipendi kucheza na watu 10, nilisema kuweni makini, tulia, dhibiti hisia zako, lakini...**

PEP Guardiola amesema Rodri aliomba msamaha kwa wachezaji wenzake baada ya kadi nyekundu aliyopewa dhidi ya Nottingham Forest na kukiri kuwa "nilikasirishwa" na kiungo huyo kwa kuifanya Manchester City kubaki na wachezaji 10.

**City walishinda mabao 2-0 kabla ya Rodri kuhusika katika ugomvi na Morgan Gibbs-White dakika moja baada ya kipindi cha mapumziko.**

Raia huyo wa Hispania alimkaba shingoni fowadi huyo wa Forest na kutolewa nje kwa kadi nyekundu, na kuwaacha City wakimenyana kwa zaidi ya dakika 40 wakiwa 10 uwanjani.

Alipoulizwa kama alikuwa na hasira na Rodri, Guardiola alisema: "Ndio. Sipendi kucheza na watu 10 kwa makosa yetu. Nilisema wakati wa mapumziko, kuweni makini. Mchezo umekuwa katika hali ngumu. Tulia, dhibiti hisia zako. Kwa bahati mbaya Rodri hakufanya hivyo.

"Natumanii Rodri atajifunza. Mchezo ulikuwa kamili kwa dakika 35 na baada ya hapo ukawa machafuko kidogo. Hilo halikuwa jukumu letu, hilo ni la uhakika. Lakini Rodri alilazimika kujidhibiti mwenyewe na hisia zake."

Guardiola pia aliulizwa kama alitarajia Rodri aombe radhi kwa wachezaji wenzake, alijibu. "Amefanya hivyo."

"Rodri ni mchezaji wa aina yake. Kyle Walker alifanya hivyo siku za nyuma. Ni hisia, wanafanya hivyo. Ujanja ni kujidhibiti. "

Rodri anatazamiwa kukosa mechi tatu kutokana na kadi nyekundu, ambayo itamfanya akose safari ya kwenda Arsenal Oktoba 8, mwaka huu.

City wana chaguo la kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo na Guardiola alisema atazungumza na klabu kuhusu uwezekano huo.

"Sijui, ni swali kwa klabu." aliongeza. "Nafikiri Rodri lazima ajifunze. Sisemi haikuwa kadi nyekundu."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 718,3

MECHI KALI

DUNDALK FC
VERSUS
CORK CITY

1 | 1.60
X | 3.72
2 | 4.63

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TEN HAG SASA ROHO KWATU MAN UNITED



**LONDON,** England

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, ameipongeza timu yake ya Manchester United baada ya kumaliza mbio zao za kupoteza kwa kuifunga Burnley Jumamosi.

'Mashetani Wekundu' hao walipata ushindi wa 1-0 wakiwa kwenye Uwanja wa Turf Moor kwa bao la Bruno Fernandes, na hivyo kuhitimisha msururu wa kupoteza michezo mitatu mfululizo, wakifungwa na Arsenal, Brighton na Bayern Munich.

Haikuwa rahisi kwa Ten Hag - ambaye alipigwa picha baada ya mchezo huo akizungumza na Mkurugenzi wa Soka, John Murtough, lakini timu yake ilipanda hadi nafasi ya nane kwenye msimamo wa ligi kwa ushindi huo, ingawa bado wako pointi nne nyuma kutoka kwenye nafasi nne za juu.

Lakini ulikuwa ushindi wa kuzuia zaidi dhidi ya wenyeji waliokuwa kwenye mechi hiyo, na ambao waligonga mwamba wa goli kupitia kwa Zeki Amdouni. Ten Hag aliwakosa wachezaji kadhaa kutokana na majeraha, akiwamo Lisandro Martinez, Luke Shaw na Aaron Wan-Bissaka kwenye safu ya ulinzi.

"Ilikuwa wazi. Bila shaka tulihitaji ushindi huo," alisema Mholanzi huyo akiiambia BBC.

"Tulikuwa na mchezo mgumu dhidi ya wapinzani wazuri. Haikuwa lazima kupoteza mchezo huu. Leo (juzi) ilikuwa lazima tushinde.

"Roho ya timu na jinsi wanavyopigana pamoja ilikuwa ya kuvutia. Ilikuwa ni timu inayoshambulia na kulinda.

"Mengi yamekuwa dhidi yetu, kama vile majeraha na maamuzi, kama vile usiku wa leo (juzi).

# Xavi: Barca imeonesha mabadiliko ya kiza

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez, amesema kutoka nyuma na kushinda kwa kikosi chake dhidi ya Celta Vigo Jumamosi kulionesha mabadiliko ya kizazi katika timu hiyo.

Robert Lewandowski alifunga mabao mawili katika dakika 10 za mwisho kabla ya João Cancelo kufunga dakika ya 89 wakati Barca walipotoka nyuma kwa mabao mawili kwenye Uwanja wa Olympic na kuwalaza Celta 3-2.

Ushindi huo wa dakika za majeruhi ulimaanisha Barcelona kuwa timu ya kwanza ya LaLiga katika misimu 14 iliyopita kushinda kutoka nyuma kwa mabao mengi ndani ya dakika ya 80, kwa mujibu wa ESPN Stats and Information.

"Ulikuwa mchezo wa kustaajabisha," alisema Xavi katika mkutano na waandishi wa habari baada ya Barca, ambayo haijapoteza katika mechi sita za LaLiga msimu huu, ilipanda kileleni mwa ligi kabla ya mechi ya Real Madrid dhidi ya Atletico Madrid jana Jumapili.

"Tuliamini hadi mwisho. Tulicheza kwa imani na ujasiri. Ilikuwa ni kurudi kwa nia ya kushinda. Usipocheza vizuri, unahitaji sifa hizi.

"Tulikuwa tukichukua hatari zaidi na zaidi, tukiwaacha wawili nyuma, kila mtu uwanjani alikuwa mchezaji wa kushambulia. Ilibidi tuchukue hatari.

"Hii inaonesha mabadiliko ya kizazi tuliyoyaona katika timu. Wachezaji hawakati tamaa 2-0 nyuma tena nyumbani, lakini kizazi hiki kinapigana hadi mwisho.

"Gavi, (Alejando) Balde, Lamine (Yamal) ... leo (jauzi) ni hatua kubwa ya kubadilika kwa tabia yetu ya ushindi. Hatujacheza soka nzuri, lakini inahusu tabia na imani kubwa."

Celta walikuwa wame gulia kwa bao la kipindi kwanza kutoka kwa Jör Strand Larsen, huku juh za Anastasios Douvikas zik zimesalia dakika 10.

Lakini mabao mawili ya wandowski, yaliyotengene na João Félix na kisha Canc yalifungua njia kwa krosi n ya Gavi kutengeneza ba ushindi kwa Cancelo.

Xavi alimuweka kiu mmoja Gavi, ambaye ali kua nafasi ya Frenkie de J aliyeumia katika kipindi kwanza kuwa katikati p yake.

345,550

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 27/09/2023 | 21:30 | St. Gallen vs BSC Young Boys | 2.55 | 3.50 | 2.26 |
| 2. 27/09/2023 | 21:30 | Catanzaro vs Cittadella | 2.22 | 3.13 | 3.13 |
| 3. 27/09/2023 | 21:30 | Como vs Sampdoria | 2.71 | 3.12 | 2.49 |
| 4. 27/09/2023 | 21:45 | Chelsea vs Brighton | 2.20 | 3.43 | 2.95 |
| 5. 27/09/2023 | 21:45 | Royal Antwerp vs KAA Gent | 2.23 | 3.45 | 2.95 |
| 6. 27/09/2023 | 22:00 | Newcastle vs Manchester City | 2.95 | 3.43 | 2.20 |
| 7. 27/09/2023 | 22:30 | Cadiz CF vs Rayo Vallecano | 2.52 | 3.14 | 2.99 |
| 8. 27/09/2023 | 22:30 | Valencia vs Real Sociedad | 2.46 | 3.08 | 3.13 |
| 9. 28/09/2023 | 19:00 | Ismaily SC vs El Ittihad Alexandria | 2.37 | 3.09 | 2.94 |
| 10. 28/09/2023 | 19:30 | Monza vs Bologna | 2.41 | 3.34 | 2.98 |
| 11. 28/09/2023 | 20:00 | Granada vs Betis | 2.85 | 3.36 | 2.49 |
| 12. 28/09/2023 | 20:00 | Orebro SK vs Utsiktens BK | 2.39 | 3.30 | 2.88 |
| 13. 28/09/2023 | 22:30 | Osasuna vs Atletico Madrid | 3.19 | 3.45 | 2.24 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 25/09/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2357 | BEC Tero Sasana vs Buriram Utd | 4.93 | 4.23 | 1.49 |
| 14:30 | 3077 | Palestine U23 vs Japan U23 | 20.34 | 7.12 | 1.10 |
| 15:00 | 1623 | Bristol City U23 vs Ipswich U23 | 1.53 | 4.38 | 4.59 |
| 15:00 | 2443 | Wigan U23 vs Burnley U23 | 1.60 | 4.48 | 3.97 |
| 15:00 | 2968 | Pyunik Yerevan vs Shirak Gyumri | 1.11 | 6.92 | 18.33 |
| 15:00 | 4780 | Pusamania Borneo vs PSM Makassar | 2.44 | 3.13 | 2.62 |
| 16:00 | 1631 | Polokwane City vs Amazulu | 2.67 | 2.82 | 2.77 |
| 16:00 | 2007 | Bangkok Utd vs Bangkok Glass | 2.05 | 3.42 | 3.02 |
| 16:00 | 4477 | National Bank vs Pyramids | 4.39 | 3.64 | 1.72 |
| 17:00 | 1121 | Ararat Armenia vs Alashkert Martuni | 2.32 | 3.15 | 2.84 |
| 17:00 | 5022 | NK Dubrava vs NK Jarun Zagreb | 1.90 | 3.37 | 3.47 |
| 17:30 | 2150 | East Bengal vs Jamshedpur | 2.35 | 3.38 | 2.57 |
| 18:00 | 3943 | FC Riga vs FK Liepaja | 1.23 | 5.49 | 9.55 |
| 19:00 | 1377 | Fakel vs Rubin Kazan | 2.41 | 3.13 | 2.82 |
| 19:00 | 1956 | CRS Salmi vs Olympique Safi | 2.19 | 2.95 | 3.10 |
| 19:00 | 2858 | Zamalek vs Arab Contractors | 1.95 | 3.29 | 3.74 |
| 19:00 | 4174 | Omonia Nicosia vs Aris Limassol | 2.90 | 3.36 | 2.29 |
| 20:00 | 2425 | IFK Varnamo vs Sirius FK | 2.16 | 3.39 | 2.83 |
| 20:00 | 3004 | Nordsjalland vs Hvidovre IF | 1.21 | 6.43 | 11.06 |
| 20:00 | 3265 | FK Napredak vs Cukaricki St | 3.73 | 3.07 | 1.94 |
| 20:00 | 3471 | Hatayspor vs Trabzonspor | 2.99 | 3.41 | 2.19 |
| 20:00 | 3649 | Halmstads BK vs Elfsborg | 3.90 | 3.54 | 1.75 |
| 20:00 | 5136 | Altay vs Bodrumspor | 3.73 | 3.33 | 1.85 |
| 20:00 | 5592 | Lillestrom SK 2 vs Skedsmo | 2.40 | 3.70 | 2.31 |
| 20:30 | 5762 | FC Aarau vs FC Vaduz | 1.77 | 3.53 | 3.84 |
| 21:00 | 1910 | Rapid Bucuresti vs CFR Cluj | 2.67 | 3.23 | 2.46 |
| 21:00 | 3724 | Panathinaikos vs AEK Athens | 2.27 | 3.13 | 3.18 |
| 21:00 | 4461 | Deportivo Municipal vs Cusco FC | 3.23 | 3.18 | 2.06 |
| 21:00 | 5981 | Jong Ajax vs FC Eindhoven | 2.61 | 3.48 | 2.35 |
| 21:05 | 4037 | Stirling University FC vs Albion Rovers | 2.95 | 3.45 | 2.12 |
| 21:15 | 2978 | GKS Jastrzebie Zdroj vs Olimpia Grudziadz | 2.43 | 3.21 | 2.65 |
| 21:15 | 3228 | Mouloudia Oujda vs FAR Rabat | 6.80 | 4.00 | 1.38 |
| 21:15 | 5995 | FC Sion vs FC Thun | 1.58 | 3.94 | 4.44 |
| 21:30 | 1319 | Deportivo Maipu vs Deportivo Madryn | 1.77 | 3.34 | 4.23 |
| 21:45 | 1164 | Wexford Youths vs Longford Town | 2.01 | 3.24 | 3.29 |
| 21:45 | 1683 | Galway United vs Finn Harps | 1.10 | 7.28 | 15.18 |
| 21:45 | 2011 | St Patricks vs Drogheda Utd | 1.62 | 3.73 | 4.43 |
| 21:45 | 4990 | Bohemians FC vs Shelbourne | 1.79 | 3.22 | 4.13 |
| 21:45 | 5531 | Dundalk FC vs Cork City | 1.60 | 3.72 | 4.63 |
| 22:00 | 1671 | Sochaux vs FC Rouen | 2.26 | 3.19 | 3.03 |
| 22:00 | 2116 | Coventry vs Huddersfield | 1.78 | 3.61 | 3.96 |
| 22:00 | 2184 | CA Platense vs Union Santa Fe | 2.60 | 2.75 | 2.85 |
| 22:00 | 4420 | Tenerife vs Espanyol | 2.52 | 3.01 | 2.77 |
| 22:00 | 4552 | Sarmiento Junin vs Belgrano Cordoba | 2.21 | 2.80 | 3.46 |
| 22:00 | 5178 | Racing Ferrol vs Zaragoza | 2.72 | 2.87 | 2.67 |
| 22:15 | 3710 | Sporting Lisbon vs Rio Ave | 1.19 | 6.20 | 12.00 |
| 22:15 | 5358 | Breidablik vs Vikingur Reykjavik | 2.95 | 3.67 | 2.05 |
| 23:00 | 1673 | Atletico Grau vs Sport Huancayo | 1.72 | 3.34 | 4.35 |
| 23:30 | 2625 | Renaissance Ezzmamra vs MAS Maghrib A Fes | 3.10 | 2.95 | 2.18 |
| 23:30 | 4589 | Orsomarso vs Bogota FC | 2.81 | 2.96 | 2.46 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# AZAM YAIONYESHA SINGIDA FG UDHAIFU IKIJIWINDA SHIRIKISHO

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Singida Fountain Gate FC, Thambo Senong, ameweka wazi changamoto inayoikabili safu yao ya ulinzi na ushambuliaji ya kutokuwa makini, jambo ambalo limewarejesha katika uwanja wa mazoezi kulifanyia kazi kuelekea mchezo wao wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Future FC ya Misri.

Singida Fountain Gate FC, ambayo ni mwakilishi pekee wa nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, inatarajia kwenda nchini Misri Jumatano wiki hii katika mchezo wa marudiano baada ya ule wa awali kushinda bao 1-0, katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

**Mchezo huo wa marudiano unatarajiwa kucheza Oktoba Mosi, mwaka huu katika Uwanja wa Al -Salam, Misri, ambapo Singida Fountain Gate FC itakuwa ikihitaji kushinda ama sare yoyote ili kutinga hatua ya makundi.**

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Thambo alisema mechi ya Azam FC ilikuwa kipimo kizuri cha kuona changamoto za timu yake, hivyo kubaini kuna tatizo la umakini husuan safu ya ulinzi na ushambuliaji.

Alisema wanaendelea kujiimarisha zaidi katika kila eneo kujiweka sawa kwa mchezo huo wa marudiano dhidi ya wenyeji wao, Future FC wakihitaji ushindi kwa ajili ya kufikia malengo yao ya kufuzu hatua ya makundi ya Shirikisho.

"Tumepoteza mechi dhidi ya Azam FC, ilikuwa mechi ya ushindani mkubwa, kipimo kizuri kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wetu wa marudiano dhidi ya Future FC, tunahitaji kushinda lazima kutumia nafasi zinazopatikana pia mabeki kutofanya makosa ya kuruhusu bao," alisema kocha huyo.

Alisema anawafahamu wapinzani wao na wanaendela kuwafuatilia katika michezo yao na wakipata nafasi wataangalia mechi ya Future FC kesho, Jumanne ambao watakuwa na mchezo Ligi Kuu dhidi ya El Dakhleya.

Mchezo huo wa Future FC dhidi ya Dakhleya utakaopigwa saa 1:00 za Misri katika uwanja wa kimatifa wa nchini humo, Cairo International Stadium).

Kikosi cha wachezaji 24 wawakilishi hao wa Tanzania katika michuano hiyo kinatarajiwa kuondoka nchini Septemba 27, mwaka huu kuelekea Misri kwa ajili ya mchezo huo wa marudiano.

## Simba yashusha presha

INATOKA UK. 24

mazoezi hadi kesho (leo) ataungana na wenzake," alisema Ahmed.

Aliongeza kuwa beki huyo anatarajia kujiunga na wenzake leo na kuingia kambini kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos ya Zambia.

"Mashabiki wa Simba wasiwe na wasiwasi juu ya hali ya beki wetu, anaendelea vizuri na ameshapata vipimo vyote na Mungu akijalia kesho (leo), atakuwa sehemu ya kikosi kitakachojiwinda kusaka ushindi dhidi ya Power Dynamos ili kufuzu hatua ya makundi," alisema Ahmed.

Simba inatarajia kuikaribisha Power Dynamos katika Uwanja wa Azam Complex, Jumapili wiki kwenye mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya ule wa awali nchini Zambi timu hizo kutoka sare ya mabao 2-2.

Simba inahitaji suluhu ama sare ya bao 1-1 au ushindi wowote ili kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.




## Mwamnyeto aahidi

INATOKA UKURASA 24

wachezaji sawa, lakini Jumamosi na Jumapili walikuwa mapumziko.

"Tuliwapa wachezaji wetu mapumziko siku ya Alhamisi baada ya mechi yetu ya Jumatano, Ijumaa walirejea na bahati nzuri nahodha wetu Mwamnyeto naye alikuja kwa mara ya kwanza baada ya kukosekana katika mechi mbili kutokana na matatizo ya kifamilia," alisema.

Michezo

Jumatatu Septemba 25, 2023

Nipashe



Rodri amtibua Guardiola

UKURASA 21

# Mwamnyeto aahidi historia Yanga CAF

## ●●● Ni wakati wakiivaa Al-Merrikh Jumamosi, aeleza alichoonya Gamondi huku...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

BAADA ya kukosekana katika mechi mbili dhidi ya Al-Merrikh na ya Ligi Kuu dhidi ya Namungo FC, Nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, amesema amerejea na atakuwa uwanjani Jumamosi kuweka historia ya klabu hiyo kutinga hatua ya makundi kwa mara ya pili baada ya miaka 24.

**Nahodha huyo amebeba dhamana ya Wananchi baada ya kudai kuwa watacheza kwa jihadi katika mchezo huo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al-Merrikh kwa ajili ya kutinga hatua ya makundi.**

Yanga wenye mtaji wa mabao 2-0 waliyoyapata ugenini, watakuwa wenyeji wa mchezo huo wa marudiano utakaochezwa Jumamosi katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi kuanzia saa 1:00 usiku.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwamnyeto alisema malengo ni kuona Yanga inafanikiwa kufuzu hatua ya makundi baada ya miaka mingi kupita.

Alisema maandalizi yanaendelea vizuri na Kocha Miguel Angel Gamondi, amefanyia kazi yaliyojitokeza kwenye mechi iliyopita ya ligi ili isijirudie katika mchezo wa marudiano dhidi ya Al-Merrikh.

"Licha ya kuwa na faida ya mabao 2-0, hatuwezi kuridhika na matokeo tuliyoyapata Rwanda, tunajiandaa, tunaenda kuipeleka Yanga makundi baada ya miaka mingi sana kutofika hatua hiyo.

"Niko vizuri, nimerejea nashukuru matatizo yameisha, tunakuja kusaka ushindi, mechi ya kwanza na Al-Merrikh nilikuwa Tanga nilikwenda kumuona mzee, lakini nilikuwa na furaha baada ya ushindi, hii ya pili dhidi ya Namungo nilikuwa nimesharejea Dar na familia yangu.

"Ilikuwa mechi ngumu kwa sababu Cedric Kazi anaifahamu Yanga ndani na nje kwa hiyo ilikuwa na changamoto sana, muhimu ni pointi tatu, Jumatatu (leo),tunaanza kazi ya kuimalizia kazi, tunawaomba wanachama na mashabiki wajitokeze kwa wingi wawe sehemu ya historia, sisi wachezaji tunasema mguu mmoja umeshaingia makundi, Jumamosi tunamalizia wa pili," alitamba.

Alisema wachezaji wote malengo yao ni kuwapa furaha mashabiki wao na kufikia malengo ya kuipambania timu ifuzu na kucheza hatua ya makundi ambayo kila Mwananchi anatamani kuona wanafikia hatua hiyo.

Aliongeza kuwa kulingana na ubora wa timu yao na wakicheza kwa kujitoa kama mechi zilizopita, hawana kitu ambacho kitawazuia kushindwa kufuzu hatua ya makundi.

Mwamnyeto alisema kocha amewaeleza safu ya ulinzi na ushambuliaji kuwa makini kulingana na wapinzani wao, Al-Merrikh hawatacheza kama ilivyokuwa mechi ya kwanza.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema baada ya mchezo wa Jumatano dhidi ya Namungo na kupata ushindi wa bao 1-0 lililowekwa wavuni na Mudathir Yahaya, wachezaji wao walipata mapumziko Alhamisi na Ijumaa kikosi kilirejea kwa ajili ya kurudisha miili ya

INAENDELEA UKURASA 23



Che Malone

# Simba yashusha presha kunusurika ajalini kwa Che Malone

**Na Saada Akida**

PRESHA ilipanda na hofu kubwa kutanda baada ya taarifa za kupata ajali kwa beki wa kati Simba, Che Fondoh Malone, kuelekea mchezo wao wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos ya Zambia, lakini klabu hiyo imewatoa hofu mashabiki wao kwa kuwaeleza yu buheri wa afya kwa mechi hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alikiri kuwa beki huyo alipata ajali usiku wa kuamka jana eneo la Mikocheni, Dar es Salaam karibu na Shule ya Feza, lakini hakuumia.

Alisema Che Malone akiwa anaendesha gari ndogo akitoka uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere alfajiri ya jana kupokea kaka zake waliokuja nchini kumtembelea, alipofika maeneo ya Mikocheni karibu na Shule ya Feza, alipata ajali baada ya kujaribu kumkwepa dereva pikipiki (Bodaboda) na gari kuingia mtaroni.

"Mchezaji alitupigia simu kutueleza na ndani ya gari hiyo ya Che Malone kulikuwa na watu wanne akiwamo mwenyewe kati ya hao ni mmoja tu aliumia kidogo. Baada ya ajali traffic walikuja kupima na kufuata taratibu zote za polisi na tukaenda Kituo cha Oysterbay na baadaye kuwapeleka hospitali ya TMJ.

"Baada ya vipimo Che Malone ameoneka yuko vizuri hajapata shida yoyote pamoja na kaka zake walitoka nchini Cameroon na wote wameruhusiwa kurudi nyumbani, kwa kuwa leo (jana) ni mapumziko hakuna

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >